Alhamisi Januari 18, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581559

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz
www.ippmedia.com
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper



**BENZEMA AMSHTAKI WAZIRI UFARANSA**

UKURASA 22

**Wageni** mataifa manane kushiriki kusimikwa Mkuu mpya wa KKKT

UKURASA 3

**Bingwa** mifupa ahadharisha staili ya kukaa kama chura na kobe

UKURASA 9



**Mch.** Mackenzie akwaa mashtaka mauaji watu 430

UKURASA 19

## KUELEKEA UCHAGUZI

# Samia aanika uteuzi utakavyokuwa CCM

• **Awaonya** wanaotegemea kugawa kanga na vitenge...*Endelea Uk. 2*



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na wanachama wa chama hicho na wananchi wa Chaani, baada ya kuweka jiwe la ufunguzi wa Tawi la CCM Chaani Masingini, Mkoa wa Kaskazini Unguja jana, akiwa katika ziara ya kukagua miradi mbalimbali ya chama. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 19

**TRUMP AENDELEZA JITIHADA KUGOMBEA URAIS MAREKANI**

BAADA ya Rais wa zamani wa Marekani, Donald Trump, kuibuka mshindi kwenye uchaguzi...

**Mtambo wa noti bandia wanaswa**

UKURASA 18



Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika, akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana, kuhusu maandalizi ya maandamano ya Januari 24, mwaka huu. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# CHADEMA yatinga polisi na barua

• **Wapinzani** wenzao wakosoa nyendo zao... *Endelea ukurasa 2&3*

**MICHEZO** SIMBA MPYA BAADA YA KUWATEMA SITA UK.24 **KATUNI** UK.6



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akipata maelezo kutoka kwa Mtaalamu wa Maabara, Abdulla Rashid Hemed, alipotembelea moja ya chumba cha uchunguzi wa matatizo mbalimbali katika jengo la huduma za dharura na maabara, baada ya kulizindua Makunduchi Wilaya ya Kusini, Mkoa wa Kusini Unguja jana. **PICHA: IKULU**

# Samia aanika uteuzi utakavyokuwa CCM

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan amebeba hoja tatu kwenye ziara yake visiwani hapa, akiwa na angalizo kuwa kazi za kuwaletea wananchi maendeleo ndizo zitakazobeba wagombea katika Uchaguzi Mkuu ujao na si kanga na vitenge.

Vilevile, ametamba kuwa CCM iko imara na haoni chama cha kukiondoa madarakani kuongoza nchi kwa sasa.

Aliyasema hayo jana alipozungumza na wanachama wa CCM na wananchi wakati wa ufunguzi wa tawi la CCM la Chaani Masingini, Mkoa wa Kaskazini Unguja ikiwa ni sehemu ya ziara zake kichama anazoendelea nazo.

"Ninataka kuwaambia jambo; tutakapopimana katika uchaguzi wetu ndani ya chama chetu, tutapimana kwa kazi za wabunge na wawakilishi walizofanya.

"Mkoa wa Kaskazini mmenionesha mambo, kipindi kilichobaki hapa ninajua nani kafanya na nani hajafanya. Hivi ndivyo tutakavyokwenda kupimana.

"Hivyo, wale walio nyuma, waanze sasa maana kimebaki kipindi kidogo tutaanza kuchujana. Ninataka kuona tathmini ya kila mbunge na mwakilishi, iwe wa jimbo au viti maalum, kazi aliyoifanya," alisema.

Aliwataka wabunge na wawakilishi kuacha mtindo wa kugawa vitenge, kanga na fedha wakati wa uchaguzi kwa kuwa anayefanya hivyo hajafanya kazi yake kikamilifu, hivyo anatoa hongo ili achaguliwe.

Badala yake, alisema kama ni zawadi zitolewe katika sherehe zikiwamo za sikukuu za kidini na si kusubiri uchaguzi ukikaribia ndipo waanze kugawa zawadi.

Alitamba kuwa mpaka sasa hajaona mbadala wa kuiondosha CCM madarakani, lakini akawa na angalizo kwa wanachama wa chama hicho kutobweteka na uimara wake.

"Waswahili wanasema 'paukwa pakawa'. Sasa pakiukwa mwingine si wanakaa. Kama mnataka kuuka kwa hiyari yenu, fanyeni fitina, kiacheni chama lakini faida yake mtakuja kuiona mbele na hasara yake mtakuja kuiona," alionya.

Mwenyekiti huyo aliwataka wanachama wa CCM kuwa na umoja na mshikamano kwa kuwa umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.

Aliwataka kuhakikisha wanaimarisha chama hasa katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu wa mwakani ili kukiwezesha kushinda.

Mwenyekiti Samia pia alionesha kuchukizwa na tabia ya Wazanzibari kutiliana fitina, kusemana, kuzushiana na kuvunjana moyo, akivitaja ni vitendo visivyo na mustakabali mwema.

Alisema hawana sababu ya kufanya hivyo kwa sababu serikali imewaletea maendeleo na kuimarisha huduma muhimu za kijamii ikiwamo afya, elimu na barabara.

Aliwasisitiza wanachama kuwa na umoja na mshikamano ili kuwapa nguvu viongozi kufanya kazi ya kuleta maendeleo nchini kwa maslahi ya taifa.

Mwenyekiti Samia alikumbusha kwamba kwa Tanzania Bara mwaka huu watakuwa na mtihani wa kuchuana na vyama vingine katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, hivyo Tanzania Zanzibar wajiandae kwa Uchaguzi Mkuu wa mwakani ili CCM isinyang'anywe mamlaka ya kuongoza dola.

"Wanakaskazini Unguja mna bahati kubwa sana maana mlezi wa mkoa wenu huu ni Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia ni Rais wa Mabunge Duniani. Sasa mkituangusha tukiona namba zinapungua, mnamwangusha mlezi wenu," alisema.

Mwenyekiti huyo wa CCM alisema amefarijika na ujenzi wa tawi hilo la Chaani Masingini na kumpongeza Mwakilishi wa Chaani kwa ujenzi huo ambao ni alama ya chama. Alisisitiza CCM inahitaji viongozi wa majimbo wanaojali uhai wa chama.

Tawi hilo lenye wanachama 1,900 ni miongoni mwa mengine 12 yaliyomo ndani ya Jimbo la Chaani na wakazi wa eneo hilo wanajihusisha na kilimo, ufugaji na biashara.

Mwenyekiti Samia pia alifungua Chuo cha Mafunzo kwa Wajasiriamali Wanawake kilichoko Mahonda, Mkoa wa Kaskazini Unguja, kilichojengwa na Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT). Kinatarajiwa kutatua changamoto ya ajira kwa vijana.


## TANGAZO LA MNADA

Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa inawatangazia wananchi wote kwamba, inatarajia kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara magari chakavu siku ya Ijumaa tarehe 02/02/2024 kuanzia saa Nne kamili (4:00) asubuhi.

| Na. | Maelezo | Mapendekezo |
|---|---|---|
| 1 | Tarehe ya Mnada | 02/02/ 2024 |
| 2 | Siku ya Mnada | Ijumaa |
| 3 | Idadi ya Magari | Matatu (3) |
| 4 | Aina ya Magari | STK 5181 Toyota Hillux(Pickup) |
| | | STK 3923 Toyota Hillux(Pickup) |
| | | SM 4271 Toyota Landcrusser |
| 5 | Mahali | Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa |
| 6 | Muda | Saa Nne Kamili Asubuhi (4:00) |
| 7 | Amana ya Mnunuzi | Asilimia Ishirini na Tano (25%) ya Thamani ya gari |
| 8 | Muda wa Kukamilisha Malipo | Siku Kumi na Nne (14) baada ya Tarehe ya Mnada |
| 9 | Muda wa kuchukua Gari | Siku Saba (7) baada ya kukamilisha malipo |

**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA KONGWA.**
**Simu: 0715 46 90 06**
**Barua Pepe: ded@kongwadc.go.tz**


# CHADEMA yatinga polisi na barua

**Na Beatrice Shayo**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimesema kimewasilisha barua Jeshi la Polisi kuhusu maandamano yaliyopangwa kufanyika Januari 24, mwaka huu, kwenda ofisi za Umoja wa Mataifa (UN), Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Dar es Salaam, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alisema maandamano hayo yatakuwa na njia mbili ya kwanza kuanzia Mbezi Mwisho na njia ya pili Buguruni.

Mnyika alisema sababu ya kwenda UN, wameona ni vyema kukimbilia katika ofisi hizo kwa kuwa umoja huo na UN ni familia ya mataifa hasa panapokuwa na tatizo ndani ya taifa.

"Tanzania imeridhia mikataba mbalimbali ya UN kuhusu haki, kutaka wananchi kuishi maisha mazuri yenye uwapo wa uchaguzi wa haki, kusikiliza maoni ya wananchi na kuheshimu mamlaka ya watu. Kwa hiyo UN ni sehemu sahihi ya kwenda baada ya mamlaka za ndani kutokutusikiliza," alisema.

Mnyika alisema maandamano hayo yaliamuliwa na Kamati Kuu ya chama na wamepeleka barua kutoa taarifa rasmi kwa mujibu wa sheria kuhusu kufanyika kwake.

Alisema katika barua hizo, wameziarifu mamlaka mbalimbali za polisi kuhusu njia zitakazotumika katika maandamano hayo ambayo yataanza saa 3:00 asubuhi na kupokewa ofisi za UN majira ya saa 8:00 mchana.

Mnyika alisema kwa mujibu wa sheria, wametoa taarifa kwa makamanda wa polisi wa mikoa Dar es Salaam, akiwamo Kamanda wa Polisi Kanda Maalum kwa kuwaandika barua ambazo wamezisambaza jana.

Alisema barua hiyo imeeleza agenda kuu ya maandamano ni kutaka kusikiliza maoni ya wananchi kuhusu haja ya kuondoa bungeni miswada ya sheria ya uchaguzi na kuitaka serikali kutengeneza mpango wa dharua ili kukabiliana na kupanda kwa gharama za maisha.

Pia alisema wanaoguswa na matatizo ya ugumu wa maisha na kupanda kwa gharama za maisha, wajitokeze kushiriki katika maandamano hayo.

"Wananchi wa Dar es Salaam wanaoguswa na upungufu wetu wa kisheria na katiba unaofanya tunakuwa na chaguzi zisizokuwa huru za serikali, kuanzia uchaguzi wa serikali za mtaa, udiwani, ubunge na urais wajitokeze kwa wingi," alisema Mnyika.

Alitoa wito kwa wananchi wanaoamini na wenye maoni mbalimbali kuhusu masuala ya nchi yanayoikabili Tanzania yaliyoelezwa na Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, popote haki zinapominywa wakutane katika vuguvugu hilo la kudai haki mwaka huu.

Mnyika alisema njia ya kudai haki ni wote wenye kuhitaji haki kukutana katika maeneo aliyoyataja kuandamana kuelekea ofisi ya Umoja wa Mataifa kupeleka ujumbe wao wa madai ya haki katika taifa lao na masuala ya msingi wanayoyahitaji ya hatua za haraka za serikali kuhusu mpango wa dharura wa kukabiliana na ugumu wa maisha na ongezeko la bei.

Alisema jambo lingine ni kuondoa miswada bungeni na badala yake kuwapo na mchakato wa maboresho ya katiba na marekebisho ya sheria itakayoweza nchi kuwa na uchaguzi huru na wa haki, nchi kuwa katika mkondo sahihi wa haki wa uhuru wa demokrasia na maendeleo ya watu.

HABARI KITAIFA

# ...Vyama vya upinzani vyakosoa uamuzi CHADEMA kuandamana

**Na Beatrice Shayo**

VYAMA vya siasa 13 vya upinzani vimetoa tamko la kukitaka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kusitisha maandamano ya amani yanayolenga kuishinikiza serikali iondoe miswada bungeni.

Vyama hivyo ni ADC, ADA TADEA, UPDP, Demokrasia Makini, SAU, CCK, NLD, NRA, TLP, UMD, AFP na UDP.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Katibu Mkuu wa DP na Mwenyekiti wa umoja wa vyama hivyo, Abdul Mluya, alisema tamko hilo linatokana na mjadala walioufanya kwa siku mbili na kukubaliana mambo kadhaa.

Alisema serikali isitishwe na maandamano ya siku moja ya CHADEMA, akisisitiza kuwa jambo la msingi kwa sasa linapaswa kuwa kushindana kwa hoja badala ya kukimbilia kufanya maandamano.

Alisema viongozi wa dini na wadau mbalimbali wa siasa na demokrasia walishiriki kutoa maoni katika mchakato wa marekebisho ya sheria zinazohusu siasa na demokrasia na wanaamini serikali haiwezi kupuuza maoni yao.

"Njia ya maandamano iliyochaguliwa na CHADEMA inatofautiana na utamaduni wa taifa kwa kuwa ina viashiria vya kuvunja amani ya nchi na kuleta mfarakano ndani ya jamii. Ni vizuri wangekubali kubishana kwa hoja au kukaa meza moja badala ya kukimbilia maandamano," alisema.

Aliongeza kuwa vyama hivyo pia vimeitaka CHADEMA kuacha alichodai mchezo wa ubinafsi kwa kuwa ilitakiwa kushirikiana nao badala ya kusimama yenyewe. Mluya alisema CHADEMA wanatakiwa kuwa na huruma na wananchi wao kwa kuwa ndio wa kwanza kupata madhara kwenye maandamano, akisisitiza yanapaswa kuwa njia ya mwisho baada ya kukata tamaa.

Katibu Mkuu wa Chama cha ADC, Hassan Doyo, alidai CHADEMA inafanya siasa za kizamani za kuandamana kwao kumepitwa na wakati.

Alidai CHADEMA inataka kuvuruga amani kupitia maandamano yasiyokuwa na msingi kwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ameruhusu uhuru wa maoni na anapaswa kupongezwa kwa mkakati wake wa kuja na 4R.

Alidai maandamano ya CHADEMA ndani yake yamebeba agenda ya siri, akifafanua "ukiitisha maandamano ambayo yana hoja ya kushinikiza jambo, hayawezi yakawa ni maandamano ya amani. Hili tunahitaji lieleweke, maandamano ambayo yanaandaliwa ndani yake yana ajenda ya siri."

Hata hivyo, mwanasiasa huyo alisema anakubaliana na hoja ya CHADEMA ya maisha magumu kwa wananchi. Kama viongozi wanapaswa kuhakikisha wanatumia nafasi yako kutatua tatizo hilo na kuhamasisha wananchi namna bora ya kupata mazao kutokana na mvua inayonyesha.

"Ili kuwaondoa Watanzania katika hali ngumu ambayo wewe kiongozi umekiri ni maisha magumu, ninawaomba Watanzania kipindi hiki ni muhimu kujielekeza kwenye kilimo ili miezi mitatu ijayo wavune mazao na kupata fedha kupitia mazao ya kibiashara," alisema Doyo.

Alisema maboresho yaliyofanywa katika miswada ikiwamo suala la ruzuku, yamefanyika ili vyama vijiendeshe kwa kuwa vingi vinashindwa kujiendesha kutokana na ukwasi.

"Tunapinga maandamano kwa sababu ni ajali, tulifanya maandamano Zanzibar. Kilichotokea ni mauaji, ndio maana tumekuja kuwaomba Watanzania wasikubali kuingia barabarani.

"Kabla ya kwenda katika maandamano watuambie maridhiano yalifikia wapi? Hii ndio hoja wenzetu mlikuwa na vikao na dola, njooni mtueleze mazungumzo yenu na CCM yamefikia wapi na yamekwamia wapi?" alihimiza.

Alisema katika maoni yao kwa kamati ya Bunge, waliwasilisha hoja ya kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi na ikifanyiwa kazi, kuna uwezekano wa kupata wabunge zaidi ya 100 kutoka vyama vya upinzani wakati wa Uchaguzi Mkuu ujao.

# Wageni mataifa manane kushiriki kusimikwa kwa Mkuu mpya wa KKKT

**Na Restuta James**

WAGENI kutoka mataifa manane, mashirika ya kimataifa ya ndani na nje na vyama vya kidini vya kikanda, wamethibitisha kushiriki kuingizwa kazini kwa Mkuu mpya wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Alex Malasusa.



Ibada ya kuingizwa kazini kwa Askofu Dk. Malasusa inatarajiwa kufanyika Jumapili katika Kanisa Kuu la Dayosisi ya Mashariki na Pwani (DMP), Azania Front jijini Dar es Salaam. Na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Katibu Mkuu wa KKKT, Mhandisi Robert Kitundu, akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu jana, alisema maandalizi ya kusimikwa kwa kiongozi huyo wa kanisa yanaendelea vizuri.

"Watakuwapo watu mbalimbali na makanisa tofauti ambayo tuna uhusiano nayo kutoka Ujerumani, Marekani, Malawi, Kenya, Burundi, Msumbiji, Afrika Kusini na Ethiopia. Wote hawa wanakuja kwa ajili ya kushiriki pamoja nasi," alisema.

Kitundu alisema KKKT imekuwa ikijihusisha na makanisa na vyama mbalimbali duniani ambavyo vimethibitisha kushuhudia tukio hilo kubwa.

"Hapa ndani tutakuwa na wageni tofauti ambao watatokea kwenye vyama mbalimbali kama Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Chama cha Biblia, makanisa ya kiprotestanti, Katoliki, Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) na viongozi wa serikali na vyama vya siasa," alisema.

Alisema washiriki wengine ni pamoja na wawakilishi wa mashirika na asasi za kiraia za kitaifa na kimataifa na kwamba, kabla ya tukio la Jumapili, kanisa litapokea salamu kutoka kwa washirika hao katika dhifa maalumu itakayofanyika keshokutwa.

Mbali na wageni hao waalikwa, Kitundu alisema tukio hilo la kuingizwa kazini kwa Malasusa litahudhuriwa na takriban maaskofu wote wa dayosisi za KKKT nchini wakiongozwa na Mkuu wa Kanisa anayemaliza muda wake, Askofu Dk. Fredrick Shoo, wa Dayosisi ya Kaskazini, ambaye ndiye atakayemsimika.

**ASKOFU MALASUSA NI NANI?**

Askofu Dk. Alex Malasusa, alizaliwa Aprili 18, 1961, katika Kijiji cha Lukinga Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya. Wazazi wake ni Mchungaji Gehaz Malasusa (sasa marehemu) na Subiliga Mwakimi. Alibatizwa na Mchungaji Amon Mtwawa Julai 1961, katika Usharika wa Igonwe, Rungwe.


## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD, TRUST RECOVERIES LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa , Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| HEAD OFFICE | FLORIAN CLAVERY RUGEMALIRA | GARI BMW X5 GH-FA30N | FLORIAN LUGEMALIRA CLAVERY | ARUSHA | 25/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | YUSUPH JULIAS MWAKIPESILE | NYUMBA | ERASTO KAMANI | PUGU BANGULO | 01/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | PASCHAL THOMAS LELO | NYUMBA (2) | 1.PASKALI TOMASI KWAYI 2.PASCHAL THOMAS LELO | 1.TEMEKE MKANGARAWE 2.YOMBO DOVYA | 02/02/2024 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | BEATRICE PETER KESSY | NYUMBA | ALEXANDER MUSSA SINDOMA | PUGU | 01/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | NGEREZA RAMADHANI NGEREZA | NYUMBA | NGEREZA RAMADHANI NGEREZA | KIVULE | 07/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | ATUPELE LABAN MWAIJIBE | NYUMBA | DR.ATUPELE LABAN MWAIJIBE | KIPUNGUNI KIPAWA-ILALA | 08/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | AMINA MUSTAFA SHIRAHE | NYUMBA | AMINA MUSTAFA SHIRAHE | KINYEREZI | 09/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | MAIMUNA ISAYA KIRINDO | NYUMBA | MAIMUNA ISAYA KIRINDO | MBEZI-KIBANDA CHA MKAA | 12/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | VENANT ERNEST THOMAS | NYUMBA | VENANT ERNEST THOMAS | DONDWE -MKURANGA | 12/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0714939933/0759648448**
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

# Mabingwa JKCI waweka kambi nchini Zambia

**Na Christina Mwakangale**

WATANZANIA tisa ambao ni madaktari bingwa wa magonjwa ya moyo kutoka Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), wamekwenda Zambia kwa ajili ya kuwafanyia upasuaji watoto 10 wanaougua magonjwa ya moyo.

Bingwa wa Upasuaji na Magonjwa wa Moyo kwa Watoto JKCI, Dk. Godwin Sharau, alibainisha hayo jana kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Julius Nyerere (JNIA) jijini Dar es Salaam wakati mabingwa hao walipoagwa kuelekea Zambia.

Alisema upasuaji huo ambao ulitarajiwa kuanza jana jioni huko Zambia, unahusisha watoto 10 ambao wana matatizo ya moyo ya kuzaliwa nayo kama vile matundu kwenye moyo.

"Sisi (JKCI) tumepiga hatua zaidi katika upasuaji wa moyo kuliko wenzetu. Tulianza tangu mwaka 2008, takribani miaka 15 sasa, wenzetu ndio wanaanza na mara nyingi husaidiwa na mabingwa wa nje.

"Tumeona kushirikiana na wenzetu na kuwapa ujuzi kutasaidia na tunaamini tutapata matokeo mazuri kwa watoto ambao walitakiwa kufanyiwa wakiwa na miezi mitatu, lakini hadi sasa wana miaka mitatu, minne hawajapata huduma hiyo," alisema Dk. Godwin.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji JKCI, Dk. Angela Muhozya, alisema kwa Tanzania ni mara ya kwanza kuweka kambi nje ya nchi na watashirikiana na Taasisi ya Taifa ya Moyo ya Zambia.

"Tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuanzisha tiba utalii, tunajitangaza na wenzetu wanakuja nchini au sisi kwenda huko kutoa matibabu.

"Katika nchi za Afrika, Tanzania ni kituo cha ubora wa tiba ya magonjwa ya moyo. Na huduma hii inasaidia sana nchi za Kiafrika ambazo zina changamoto ya kufuata huduma nje ya bara," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema upasuaji huo ni katika kambi ya siku tatu na itakuwa na mabingwa kutoka JKCI, baada ya awali kuanza kwa huduma ya uchunguzi kwa watoto wanaotakiwa kufanyiwa upasuaji Zambia.

Balozi wa Tanzania nchini Zambia, Lt. Jenerali Edward Mkingule, alisema historia inawekwa nchini kutokana na kufanikisha diplomasia ya kiuchumi, ikiongozwa na Rais Samia.

"Kambi hii ya siku tatu Zambia kwa wazalendo hawa ni heshima kubwa. Tunawaaga hapa JNIA wakielekea Zambia kushirikiana na majirani zetu," alisema balozi huyo.



Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi akikagua mradi wa ujenzi wa nyumba 5000, zinazojengwa na serikali kupitia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), katika Kijiji cha Msomera, wilayani Handeni mkoani Tanga jana, kwa ajili ya wananchi wanaohamia kijijini hapo kutoka Hifadhi ya Ngorongoro, mkoani Arusha. **PICHA: JENNIFER GILLA**

# Serikali yaonya upotoshaji wanaohama Ngorongoro

**Na Jenifer Gilla**

SERIKALI imesema upotoshaji unaofanywa na baadhi ya wanaharakati kwa wananchi wanaohama kwa hiari katika Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA), unawatia hofu na kurudisha nyuma utekelezaji wa shughuli hiyo.

Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo na Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, alitoa kauli hiyo jana katika Kijiji cha Msomera, wilayani Handeni, mkoani Tanga wakati akizungunza na waandishi wa habari.

Waandishi wa habari wako katika ziara ya kushuhudia maendeleo ya miradi inayotekelezwa kwenye eneo wanakohamia wananchi hao, hasa makazi.

Matinyi alisema kutokana na hali hiyo, serikali inaendelea kutoa elimu kwa jamii hiyo kuhusu umuhimu wa kuhama katika eneo hilo ili kuwa huru kufanya shughuli za maendeleo kama vile kilimo na biashara, jambo ambalo haliruhusiwi ndani ya hifadhi hiyo iliyoanzishwa kisheria miaka 65 iliyopita.

Alisema baadhi ya wanaharakati wamekuwa wakiwapa wananchi taarifa za uongo kuwa wakihamia katika kijiji hicho, mifugo yao itapata chanjo yenye sumu inayotolewa na serikali na kusababisha vifo.

Matinyi alisema taarifa nyingine potofu inayosambazwa na watu hao ni kuwa uhamishwaji wa wananchi hao unatumia nguvu na kukiuka haki za binadamu, hali inayoleta taharuki kitaifa na kimataifa.

Alisema lengo la serikali kuhamisha wananchi ni kuwaondoa katika maisha duni kwa kuwapa fursa ya kufanya shughuli za maendeleo, huku ikiimarisha hifadhi hiyo ambayo uhai wake kiikolojia umeendelea kudhoofishwa na shughuli za kibinadamu.

Alisema kuwapo wananchi hao katika hifadhi una athari kubwa kwao kama vile mifugo kuambukizwa magonjwa na kuliwa na wanyamapori.

"Lakini kuendelea kuongezeka kwa mifugo hiyo kunaathiri utalii kwa sababu watalii wanalalamika kulipia kuona wanyamapori, lakini matokeo yake wanakutana na mifugo," alisema.

Alibainisha kuwa katika awamu ya pili ya mradi huo, mpaka kufikia Januari 12, mwaka huu, kaya 525 zilikuwa zimejiandikisha kuhama kwa hiari. Kati yake, 126 zimeshahama na wanategemea kupokea kaya 72 kesho.

Alisema wananchi hao wanapohamia katika eneo hilo, wanapewa magunia mawili ya mahindi kila baada ya miezi mitatu kwa muda wa miezi 18 pamoja na huduma zote muhimu za kijamii kama vile elimu, afya, mawasilliano na maji.

Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi - Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini wa NCAA, Lilian Magoma, alisisitiza wanazingatia haki za binadamu, sheria na utu katika kuwahamisha kwa hiari wananchi hao tofauti na taarifa zinazosambazwa.

Kamishna Lillian alisema licha ya kujengewa nyumba na kuwekewa huduma muhimu za kijamii, serikali anaipa kila familia Sh. milioni 10 kwa ajili ya kuimarisha maisha yao.

Alisema pamoja na changamoto hizo, hamasa ya wananchi kuhama katika hifadhi hiyo ni kubwa na wanatarajia kuhamisha zaidi ya kaya 20,000.

Alisema kati ya hizo, 10,000 zinatarajiwa kuhamia maeneo yaliyoandaliwa na serikali ambayo ni vijiji vya Msomera kilichoko Halmashauri ya Handeni, Kitwai kilichoko Simanjiro na Saunyi kilichoko Kilindi na 4,000 watahamia maeneo waliyochagua wenyewe.

Alisema ili kukidhi matakwa ya idadi ya waliojiandikisha katika awamu hii ya pili ya mradi, serikali inatarajia kujenga nyumba 5,000 katika vijiji hivyo.

Magoma alisema mpaka sasa nyumba 364 zimeshakamilika na 636 ziko katika hatua za mwisho na 1,000 zinatarajiwa kukamilika mwaka huu 2024.

Diwani wa Ngorongoro aliyehamia katika eneo hilo la Msomera, Johannes Tiamas, alisema uhuru wa kufanya wanachotaka walionao wananchi wa Msomera umewafanya kuwa na mawazo mapana ya maendeleo kulinganisha na waliobaki hifadhini.

Alisema wengi wa wananchi hao wanamiliki mifugo yao, kilimo na biashara, jambo ambalo awali halikuwapo kutokana na kuishi hifadhini.

"Huku (Msomera) mifugo inaongezeka kwa kasi kwa sababu haidhuriwi na wanyama wakali na hatuitegemei katika kuendesha maisha.

"Tuna vyanzo vingi vya kutuingizia fedha, tuna kilimo. Ukiishiwa fedha, unauza maharage au mahindi tofauti na Ngorongoro mifugo ilikuwa ndio chanzo pekee cha kupata fedha," alisema.

Tiamas aliomba serikali kuongeza kasi ya utoaji elimu kwa wenzao walioko Ngorongoro ili wahamie katika eneo hilo na kuboresha maisha yao kama walivyo Watanzania wengine.

Mmoja wa wakazi wa Msomera, Meng'atei Molel, alisema tangu alipohamia katika kijiji hicho Julai 2020, maisha yake yamebadilika kwa kiasi kikubwa ikiwamo kumiliki hati ya eneo analoishi, jambo ambalo Ngorongoro haliwezekani.

Alisema fedha aliyopewa na serikali, aliitumia kununua mifugo na sasa anamiliki ng'ombe na mbuzi 50. Akiwa Ngorongoro, hakuwa na uwezo wa kumiliki mali hizo japo aliishi jamii ya wafugaji.

"Fedha zile tumewekeza katika kilimo na mwaka huu tunategemea mavuno ya kutosha kwa kuwa mvua imenyesha ya kutosha, tunategemea kupata mazao ambayo tutauza na mengine tutatunza kwa ajili ya familia," alisema.

Mwanafunzi wa Kidato cha Pili katika Shule ya Sekondari ya Msomera, Nemali Minga'ti, alisema alimaliza darasa la saba akiwa Ngorongoro. Baada ya kwenda huko, alijiunga na elimu ya sekondari moja kwa moja, hivyo taarifa kuwa eneo hilo halina huduma ya elimu si sahihi.

Mwanafunzi huyo aliomba serikali kuharakisha ujenzi wa mabweni ili wasome kwa utulivu.

Edina Yohana, mkazi mwingine wa eneo hilo, alisema kikubwa anachofurahia ni uhuru wa kutembea mchana na usiku, akipata muda wa kutosha kufanya shughuli za maendeleo.

Alisema wakiwa hifadhini, walilazimika kuingia ndani na kufungia mifugo yao giza lilipoingia kwa kuhofia kudhuriwa na wanyama wakali wakiwamo simba na tembo kwa kuwa ndio muda wanaopenda kutembea kusaka malisho.

## 'Idadi wanafunzi wanaoripoti kidato cha kwanza hairidhishi'

**Na Hamisi Nasri,** NANYUMBU

SERIKALI wilayani Nanyumbu, mkoani Mtwara imetishia kuwasweka rumande wazazi na walezi watakaoshindwa kuwapeleka watoto wao waliochaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari baada ya mahudhurio kutoridhisha.

Agizo hilo limetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Nanyumbu, Dk. Stephen Mwakajumilo baada ya ziara ya shule mbalimbali za wilaya hiyo kuangalia mahudhurio ya wanafunzi wa kidato cha kwanza na kushuhudia idadi ndogo ya walioripoti tangu zilipofunguliwa Januari 7, mwaka huu.

Alisema serikali haitovumilia au kuona mtoto wa mzazi yeyote wilayani humo amefaulu na kujiunga na elimu ya sekondari halafu anashindwa kwenda shuleni kwa kisingizio cha mzazi kutomtimizia mahitaji ya msingi vinginevyo serikali itamchukulia hatua za kisheria.

Alimtaka kila mwanafunzi aliyechaguliwa kujiunga na sekondari aripoti shule na kuanza masomo hata kama hajapata sare, cha msingi awe na madaftari na kalamu na akiwa shuleni mzazi au mlezi ataendelea kujitafuta na kununua vifaa hivyo.

Alisema watendaji wa kata na vijiji vyote vilivyopo wilayani humo wawahamasishe wazazi na walezi, watoto waripoti shule na kuanza masomo hata kama watakuwa hawajakamilisha vifaa vinavyohitajika.

"Sisi kama wilaya ya Nanyumbu tutahakikisha watoto wote waliochaguliwa elimu ya sekondari wanaripoti shuleni kuanza masomo na mzazi au mlezi ambaye mtoto wake amefaulu na kushindwa kumpeleka shuleni atachukuliwa hatua kali za kisheria," alisema Mwakajumilo.

Alisema serikali imetoa fedha nyingi wilayani Nanyumbu kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ikiwamo upande wa sekta ya elimu kwa kujenga vyumba vya madarasa na ununuzi wa vifaa vya kujifunzia na kujisomea ili kila mwanafunzi atakayechaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari asoma katika mazingira rafiki.

Alikumbusha wazazi kutambua kwamba elimu ndio urithi wa mtoto hivyo anapaswa kupewa elimu kwa kupatiwa mahitaji yote ya msingi yatakayomwezesha kupata elimu katika mazingira rafiki.

Wilaya ya Nanyumbu ina jumla ya wanafunzi 2,922 waliochanguliwa kujiunga na elimu ya sekondari kwa mwaka huu na hadi sasa hali ya maudhurio ni ndogo.

Mwakajumilo alisema serikali imejenga vyumba vya madarasa vya kutosha ili kila mtoto aweze kusoma akiwa katika chumba cha darasa na chenye kukidhi ubora ili kuondoa changamoto ya wanafunzi kusoma katika mazingira yasiyo rafiki.

# Jela miaka 35 kumbaka mdogo wake na kumwambukiza VVU

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Geita imemhukumu Deoratias William (43), kifungo cha miaka 35 jela kwa makosa ya kubaka na kumwambukiza virusi vya Ukimwi kwa makusudi mdogo wake mwenye umri wa miaka 17.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa mahakama hiyo, Nyakato Bigirwa, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha makosa yote mawili.

Hakimu Bigirwa alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na kwa watu wengine wenye tabia za kuwabaka wadogo zao. Alisema upande wa mashtaka ulikuwa ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Kabula Benjamin, ambaye alipeleka hapo mahakamani mashahidi watano na kielelezo kimoja ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa alitenda makosa hayo.

Hakimu Bigirwa alisema shahidi wa kwanza upande wa Jamhuri ambaye ni mwathirika wa tukio hilo alidai mahakamani kuwa alikuwa akiishi na kaka yake ambaye ni mshtakiwa kuanzia mwaka 2018 hadi 2023.

Alidai siku ya tukio mshtakiwa aliingia chumbani na kumbaka mdogo wake na kumwambukiza virusi vya Ukimwi na baada ya tukio hilo alimpeleka kituo cha afya Katoro, alipofanyiwa uchunguzi wa kidaktari aligundulika ana maambukizi ya virusi vya ugonjwa huo.

Aidha, alisema mwathirika alienda kutoa taarifa kwa ndugu zake na mshtakiwa alikamatwa na kufikishwa kituo cha polisi Katoro na baadaye alipelekwa kituo cha polisi Geita kisha kufikishwa mahakamani.

Hakimu Bigirwa alisema ameangalia ushahidi wa pande zote na kugundua kuwa upande wa mashtaka umethibitisha makosa yote mawili pasipokuacha shaka yoyote. Na mahakama hiyo inamtia hatiani kwa makosa yote mawili.

Mshtakiwa alipopewa nafasi ya kuzungumza, aliomba kupunguziwa adhabu kwa kupiga magoti kuwa ana virusi vya Ukimwi, pia ana watoto wanamtegemea.

Upande wa Mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Kabula Benjamin, ulidai kuwa hakuna kumbukumbu za makosa ya nyuma ya mshtakiwa, hata hivyo uliomba mahakama kutoa adhabu kwa mujibu wa sheria.

Hakimu Bigirwa alisema mahakama inamhukumu mshtakiwa kosa la kwanza miaka 30 jela na kosa la pili miaka mitano na adhabu zote zinatekelezwa kwa pamoja.

Awali, akisoma hati ya mashtaka Wakili wa Serikali, alidai katika tarehe tofauti kati ya mwaka 2018 na 2023 mtaa wa Mombasa Raha, Kata ya Butundwe, Mkoa wa Geita mshtakiwa alimbaka mdogo wake msichana na kumwambukiza virusi vya Ukimwi kwa makusudi.



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, akijibu hoja kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii (hawapo pichani), walipokutana bungeni jijini Dodoma jana. Kulia ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mhandisi Cyprian Luhemeja. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Mfumo kuwezesha majaji kusikiliza kesi hata nje ya nchi

**Na Grace Gurisha**

JAJI Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma, amesema mfumo mpya wa ki-elektroniki wa Kuratibu Uendeshaji na Usimamizi wa Mashauri (Electronic Case Management System–e-CMS), utakuwa na uwezo wa kuwapangia majaji na mahakimu mashauri hata wakiwa nje ya nchi na kuyasikiliza.

Aidha, majaji na mahakimu watakaopangiwa mashauri hayo watakuwa na uwezo wa kusoma nyaraka zote za shauri zilizo katika nyaraka laini zinazopatikana kwa njia ya ki-elektroniki wakiwa pahali popote. Profesa Juma alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, kuhusu maadhimisho ya wiki na siku ya sheria kwa mwaka huu ambayo kaulimbiu yake ni 'Umuhimu wa Dhana ya Haki kwa Ustawi wa Taifa: Nafasi ya Mahakama na Wadau Katika Kuboresha Mfumo Jumuishi wa Haki Jinai'.

Alisema mfumo huo unalenga kutoa huduma mbalimbali za kielektroniki, utaruhusu pia majaji na mahakimu kuandika hukumu na mienendo ya mashauri moja kwa moja kwenye mfumo.

"Mfumo huu utawafanya majaji na mahakimu waingie tu mahakamani kusikiliza mashauri bila kuandika, akili bandia (Artificial Intelligence) ndiyo utakuwa unafanya kazi yake, lugha ndiyo itachaguliwa kwamba ni ipi itumike, kwa hiyo hakutakuwa na ucheleweshaji wowote."

"Mahakama ya Tanzania ilishirikiana na Kampuni ya Almawave ya Italia na kujenga mfumo, uliotumia Artificial intelligence kufundisha lugha ya Kiswahili na Kiingereza cha kisheria na kimahakama ili mfumo usaidie kufanya unukuzi (transcription) na pia kutafsiri (translation). Mfumo huu umeshafungwa kwa awamu ya kwanza katika mahakama 11," alisema Profesa Juma.

Akizungumzia maadhimisho hayo, Profesa Juma alisema yataanza Januari 24, hadi Januari 30, 2024 katika viwanja vya Mwalimu Nyerere Square, Jiji la Dodoma na uzinduzi rasmi utafanyika Januari 27, kwa matembezi, mgeni rasmi atakuwa Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson na kilele ni Februari Mosi, kwenye viwanja vya Chinangali jijini humo. Mgeni Rasmi anatarajiwa kuwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

"Lengo la maonesho haya ni kuwaonesha wananchi uwekezaji uliofanywa na faida kubwa inayopatikana kutokana na ubora, ufanisi na gharama ndogo ya haki itakayopatikana mahakamani na pia waone mifumo mipya iliyofungwa na mahakama ambayo inawasaidia wao," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali itoe tamko mahususi kuhusu michango katika elimu

**KATIKA** toleo la jana la gazeti hili, kulikuwa na habari kuhusu shule moja ya sekondari ambao imetangaza kuwa kila mwanafunzi anayeripoti kuanza masomo shuleni hapo, kuchangia Sh. 65,000 kwa ajili ya uendeshaji wa shule.

Fedha hizo zimeainishwa kwenye fomu ya kujiunga zikiwamo pia fedha za tahadhari (Sh. 5,000), nembo (Sh. 5,000) na kitambulisho cha shule Sh. 5,000 hivyo kufanya jumla ya fedha anazotakiwa mwanafunzi kuchangia kuwa Sh. 80,000.

Hilo limebainika ikiwa ni wiki moja tangu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, apige marufuku shule kuweka michango ya lazima inayowanyima watoto fursa ya kwenda shuleni. Katika agizo lake alilolitoa Januari 9, mwaka huu, Waziri Mkenda alisema ni marufuku kwa shule yoyote kuweka michango ya lazima ambayo mzazi au mtoto asipotoa, mtoto atakatazwa kwenda shuleni.

Pamoja na agizo hilo ambalo pia linasisitiza mtoto asirudishwa nyumbani kwa kutochangia dawati au chochote, Shule ya Sekondari ya Wasichana Shinyanga, imekiuka au kukaidi agizo hilo. Kwa maneno mengine, shule hiyo imekaidi agizo la waziri kuhusu michango ya lazima kwa wanafunzi, hivyo kwenda kinyume na mpango wa serikali wa kutoa elimu kwa wanafunzi bila malipo.

Mbaya zaidi, hata ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga imesimamia uamuzi huo kuwa ni sahihi kwa madai kwamba ni kwa mujibu wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwamba kila mwanafunzi anatakiwa kuchangia Sh. 65,000. Pamoja na kudaiwa kuwa ni agizo la TAMISEMI, Waziri mwenye dhamana, Mohamed Mchengerwa amesema hakuna mchango wowote na mtoto yeyote haruhusiwi kupokewa kwa kumwekea masharti na kwamba anatakiwa aende shuleni na aanze masomo mara moja.

Mbali na kukana kuwapo kwa michango hiyo, Mchengerwa alibainisha kuwa serikali inatoa mabilioni ya shilingi kila mwezi na kwamba mtoto anayekwenda shuleni kokote nchini, apelekwe bila masharti yoyote huku akisisitiza kuwa atafuatilia ni kwa nini shule hiyo inaendelea kutoza michango ilhali serikali ilishatoa tamko.

Kuwapo kwa suala hili kuifanye TAMISEMI na viongozi wengine wenye dhamana ya elimu kuamka na kuanza kufuatilia shule kama hizi zinazotoza michango kwa wanafunzi kinyume cha mipango ya serikali.

Wahenga wanasema panapofuka moshi pana moto, kwa mantiki hiyo kuna uwezekano mkubwa wa kuwapo shule za namna hiyo ambazo zinatoza michango kinyemela, hivyo kukiuka maagizo ya serikali ya kutaka wanafunzi wanaojiunga na shule za serikali kutolipa mchango wowote kwa kuwa ilishatangaza kwamba elimu inayotolewa hadi kidato cha sita ni bure.

Iwapo uchunguzi utafanyika na kubainika kuwapo shule zaidi zinazotoza michango hiyo, wahusika wote kuanzia maofisa elimu ngazi ya kata hadi halmashauri wachukuliwe hatua. Kuwapo kwa jambo hilo na viongozi katika ngazi husika kulifumbia macho ni kwamba wanashiriki kwa namna yoyote kubariki kufanyika kwake.

Ni vyema pia mawaziri wenye dhamana na elimu pamoja na TAMISEMI wakatoa tamko ambalo litawezesha kuondolewa kwa mkanganyiko huo ambao baadhi ya maofisa wanaosimamia elimu katika maeneo yao wanatoa kauli zinazokinzana na uamuzi wa serikali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Kuvuja mitihani ya wataalamu wa afya mafunzoni ni kuchezea uhai

**AFYA** bora ni moja ya haki ya msingi ya binadamu na kiungo muhimu cha kufanikisha ajenda ya Malengo 17 ya Kimataifa ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ifikapo mwaka wa 2030, hasa lengo namba tatu.

Lengo namba tatu linataka kuhakikisha watu wanakuwa na afya nzuri na pia kuhimiza hali njema kwa watu wote, katika umri wowote. Hivyo, huduma bora za afya ni muhimu ziwepo kwa kila mtu.

Wakati kukiwa na himizo la huduma bora za afya, kumekuwapo na changamoto ambayo kama hatua kali za kisheria hazitachukuliwa, huenda ikahatarisha afya za Watanzania kwenye baadhi ya maeneo.

Hiyo inatokana na kuwapo kwa mchezo wa uvujishaji wa mitihani au udanganyifu kwa watu wa kada ya afya unaoweza kusababisha baadhi ya wahitimu wa kada hiyo kutokuwa na sifa za kutoa huduma za afya.

Mara kadhaa kumekuwapo na taarifa za kufutwa kwa matokeo ya mtihani ya wahitimu wa kada hiyo, kutokana na kuvuja kwa mtihani, kitendo ambacho wanaweza kupata ufaulu usioendana uwezo wao.

Kwa mfano mmojawapo ni wa juzi ambao umetangazwa na Wizara ya Afya kwamba imefuta matokeo ya mtihani wa usajili na leseni ya Baraza la Uuguzi na Ukunga ya wahitimu 1,300.

Wahitimu hao ni wale wenye elimu ngazi ya stashahada, huku sababu kubwa za kuwafutia zikatajwa kuwa ni baada ya matokeo hayo kuvuja, na kwamba wajipange upaya kurudia mtihani.

Taarifa zaidi za kuhusu kurudiwa kwa mtihani huo zitatolewa na baraza na wanatakiwa kujiandaa kwa kufuata taratibu, kanuni na sheria ili wafanye upya mtihani huo.

Uamuzi wa Wizara ya Afya unalenga kuhakikisha baraza linathibitisha wataalamu wenye sifa stahiki kulingana na taaluma zao kutoa huduma bora za matibabu kwa wagonjwa na kuzingatia usalama wa mteja anayetegemea kupata huduma za uuguzi na ukunga.

Kwa kuwa Baraza la Ukunga na Uuguzi Tanzania chini ya Wizara ya Afya, lina jukumu kusimamia taaluma za wauguzi na wakunga, ninadhani linatakiwa kumaliza vitendo vya udanganyifu kwenye mitihani.

Ninaamini kwamba kuvuja kwa mitihani ni hatari, ni sawa na kucheza na afya au uhai wa Watanzania, kwani kama mitihani inavuja, maana yake ni kwamba kunakuwa na wataalamu ambao wanakwenda kuumiza watu.

Watakuwa wamefaulu, lakini wasio na uelewa wa huduma wanayokwenda kuitoa kwenye jamii. Kimsingi, hawawezi kuelewa kikamilifu jinsi wanavyomtibu mtu.

Kuvujisha mitihani katika fani inayohusisha uhai wa watu ni hatari, ambayo haipaswi kuvumiliwa kwani Watanzani wengi wanaweza kuumia kupitia mazingira hayo.

Wataalamu wa afya ndio ambao kwa kiasi kikubwa wanaokoa maisha ya binadamu, lakini inapofanyika mikakati ya kumfanya mtaalamu afaulu bila vigezo, anaweza kusababisha maafa huko atakakopangiwa kazi.

Kwa ujumla ni kwamba, kuvujisha mitihani hasa wa wauguzi, ni kuwaandaa wauguzi ambao watakuja kufanya kazi za kitabibu chini ya kiwango na hivyo kuweka rehani maisha ya wagonjwa.

Ni vyema mamlaka husika kutafuta dawa ya kudumu ya kuziba mianya yote inayochangia kuvuja kwa mitihani, ili kulinda afya za Watanzania, hasa kwa kuzingatia kwamba kazi hiyo ni miongoni mwa kazi za wito.

Kama mtu hana wito na kazi hiyo, ni vyema asiisomee, kwani huenda ni miongoni mwa hao wanaotafuta ufaulu kwa njia zisizo halali, ambao mwisho wa siku anakwenda kuhatarisha afya za Watanzania.

## TIC yazunguka mikoa kuhamasisha uwekezaji

**Na Joseph Mwendapole**

MAOFISA wa Kituo cha Uwekezaji Nchini (TIC), wameanza kampeni ya kuzunguka nchi nzima kuhamasisha wawekezaji na Watanzania kuchangamkia fursa za uwekezaji nchini badala ya kuachia wageni.

TIC pia imesema kwenye kampeni hiyo inaelimisha umma fursa za uwekezaji ziko kwa ajili ya Watanzania pia kwa kuwa baadhi ya watu wanadhani uwekezaji unawahusu wageni pekee.

Akizungumza na gazeti hili kwenye mahojiano ya simu akiwa mkoani Manyara, Meneja Uhamasishaji Uwekezaji wa ndani wa TIC, Felix John, alisema awamu ya kwanza watazunguka mikoa 18.

Alisema mpaka sasa wamepita mikoa ya Mwanza, Singida, Arusha, Manyara, Geita, Singida na Tabora na leo wanatarajia kuanza kampeni hiyo kuanzia Kilimanjaro na kuendelea mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe na Mtwara.

"Tumepita kwenye hoteli mbalimbali kila tunakopita na wamiliki wameonyesha nia ya kujisajili TIC baada ya kuwaeleza kuhusu vivutio mbalimbali vya uwekezaji watakavyopata iwapo watajisajili na TIC," alisema.

"Pia tumepata nafasi ya kupita kwenye kiwanda kikubwa cha kutengeneza mbolea cha Minjingu ambacho kwa asilimia 80 kinamilikiwa na Mtanzania na kinauza pia mbolea ndani na nje ya nchi."

John alisema kiwanda hicho kwa sasa kiko kwenye upanuzi ili kiweze kuongeza uzalishaji kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya mbolea nchini na nyingine kuuza kwenye masoko mbalimbali ya nje ya nchi.

Alisema mabadiliko ya Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 2022 yametoa vivutio vya kikodi kwa wawekezaji watakaopanua viwanda vyao na wengi wameshaanza kuitumia fursa hiyo kwenye mikoa mbalimbali nchini.

Hivi karibuni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji), Profesa Kitila Mkumbo, aliwaambia waandishi wa habari kwamba kampeni ya kitaifa ya kuhamasisha uwekezaji wa ndani itaanzia Januari na inatarajiwa kuhitimishwa mwezi Septemba, mwaka huu.

Aidha, alisema Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alizindua rasmi kampeni ya kitaifa ya kuhamasisha uwekezaji kwa lengo la kutoa msukumo maalum kwa Watanzania kuchangamkia fursa za uwekezaji zilizoko nchini.

Alisema kama sehemu ya utekelezaji wa kampeni hiyo, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji imeamua kuufanya mwaka 2024 kuwa mwaka wa kitaifa wa kuhamasisha uwekezaji nchini hasa kwa Watanzania.

Alisema katika kutekeleza mpango huo, kuanzia Januari hadi Februari, mwaka huu ofisi yake kwa kushirikiana na TIC wataendesha kampeni maalum nchi nzima kupitia vyombo mbalimbali vya habari.

Alisema, baada ya kukamilika kwa kampeni ya vyombo vya habari, kampeni hiyo itaendelea kwa mwaka mzima kupitia semina na makongamano katika mikoa na wilaya zote nchini na itahitimishwa na kongamano la kitaifa la uwekezaji.

Aidha, kampeni hiyo ina malengo saba mahsusi ya kutoa elimu ya uwekezaji kwa Watanzania kwamba ili uwekeze lazima uwe tajiri.

# Visima vyawekwa dawa ili kutokomeza kipindupindu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MAABARA ya Maji mkoani Shinyanga, imeanza kuweka dawa kwenye visima katika maeneo yote ya mkoa huo ili kuua vijidudu vyenye vimelea vya kipindupindu.

Mpaka sasa dawa ya kuua wadudu imewekwa katika visima vya maji 22, pamoja na kuchukua sampuli 12 ili kuzipima kama vina vimelea vya vijidudu vinavysababisha kipindupindu na sampuli tisa zimebainika kuwa na vimelea hivyo.

Meneja Ubora Maabara ya Maji Mkoa wa Shinyanga, Michael Kayanda, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuwa baada ya kubaini tatizo hilo imebidi kuweka dawa kwenye visima ili kukabiliana na ugonjwa huo.

Alisema wamejipanga kuendelea kuchukua sampuli kwenye visima vya maji katika maeneo yote pamoja na kuweka dawa ili kuhakikisha wananchi wanaendelea kuwa salama.

Meneja Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), mkoani Shinyanga, Mhandisi Juliety Payovela, aliwataka wananchi kwa kipindi hiki chenye ugonjwa huo wasitumie maji ya kwenye visima, bali watumie majisafi na salama kutoka Mradi wa Ziwa Victoria.

Aidha, alitolea mfano katika Kata ya Kagongwa wilayani Kahama, kwamba eneo hilo kuna mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria, lakini wananchi hawatumii maji hayo na kwenda kuchota kwenye visima ambavyo vipo jirani na vyoo na mvua zikinyesha maji ya kwenye vyoo hutiririka kwenda kwenye visima vyao.

"Hii ndiyo sababu eneo hilo limebainika la kwanza kuwa na mlipuko wa ugonjwa huu hatari mkoani hapa kwani visima vyao vingi vipo jirani na vyoo, ambapo kisheria kisima kina paswa kuwa umbali wa mita 60 kutoka kwenye choo," alisema Mhandisi Payovela.

Alisema idadi kubwa ya visima vya wananchi vimechimbwa hadi mita 10 na mvua ikinyesha maji ya choo yanaingia kwenye visima na kuhatarisha afya za watumiaji wa maji hayo.

Baadhi ya wananchi wa Shinyanga waliomba serikali kupitia wataalamu wa afya, kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kwa kufanya mikutano ya hadhara na hata kupita na matangazo ya kwenye magari kila mtaa, kuwapatia elimu namna ya kukabiliana na ugonjwa huo.



Kaimu Mkurugenzi wa Ufuatiliaji na Uzingatiaji wa Sheria wa Shirika la Viwango nchini (TBS), Dk. Candida Shirima (wa pili kushoto), akizungumza kwenye mafunzo na wadau wa mabati Dar es Salaam jana. Wengine ni Ofisa Udhibiti Ubora wa shirika hilo, Nyabuchwenza Methusela (kushoto), Kaimu Meneja wa TBS Kanda ya Mashariki, Francis Mapunda (kulia), Mkurugenzi wa Uagizaji Bidhaa Nje wa TBS, Gervas Kaisi na Mkurugenzi wa Uandaaji Viwango, David Ndibalema. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Ofisi Wakili Mkuu wa Serikali yaanza kwenda kiteknolojia

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

OFISI ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS), imeanza kutumia Mfumo wa Mashauri wa Mahakama Kuu Tanzania wa Kielektroniki (e-CMS) kuongeza matumizi ya TEHAMA, uwazi, uwajibikaji na upatikanaji wa taarifa kwa haraka kwa lengo la kujenga imani kwa wananchi kuhusu utendaji kazi wa vyombo vinavyotoa haki.

Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Mark Mulwambo alisema hayo mjini hapa wakati akifungua mafunzo elekezi kuhusu mfumo huo na utunzaji wa nyaraka za serikali.

Mafunzo hayo yaliwahusisha washiriki 27 kutoka ofisi hiyo pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kubadilishana uzoefu kwenye masuala ya usajili wa mashauri, utunzaji wa kumbukumbu za kielektroniki na namna nzuri ya kuwahudumia wateja wa ndani na nje.

Mulwambo alisema ofisi yake imeona ni muhimu kwa watumishi kupata mafunzo kuhusu mfumo huo ili waweze kuutumia kwa pamoja na kusomana na mfumo wa Usajili wa Mashauri wa ofisi yake (CIMS).

Alisema lengo ni kuboresha utendaji kazi, kuongeza tija na ufanisi katika usajili, matumizi na uendeshaji wa mashauri baina ya mahakama, ofisi ya wakili mkuu wa serikali, wadau na wananchi.

"Lengo la Mfumo wa e-CMS ni kufanikisha utoaji wa taarifa kwa wahusika kuwa shauri lao limesajiliwa na kupangiwa jaji au hakimu," alisema Mulwambo.

Kadhalika, umetoa mwanya wa kujumuisha taarifa za taasisi nyingine za serikali ili ziweze kutumika na kusomana na utaendana na taratibu za utendaji wa mahakama.

Alisema chini ya mfumo huo, majaji wanaandika mwenendo wa mashauri kwenye mfumo badala ya kuandika kwenye majalada na kurahisisha upatikanaji wa mwenendo wa mashauri ya mahakama.

Mulwambo alisema mfumo huo unapanga mashauri kwa kila jaji badala ya mmoja kuwa na mashauri mengi au machache, umefanikisha usajili wa namba ya utambuzi wa kesi ambayo haijirudii na kutumiwa na mahakama nyingine.

Alisema mfumo huo umesajili taarifa za mashauri ya Mahakama ya Rufani, hapo awali haikuwapo na umetambua na kuruhusu matumizi ya taarifa kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).

Pia umetambua na kuruhusu matumizi ya taarifa kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS), Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS) na taarifa za taasisi nyingine.

Alisema pia umetambua na kubaini usajili wa mawakili na waendesha mashtaka halali kwa kuwatambua kwa namba zao.

"Tumefurahishwa na Mahakama Kuu ya Tanzania kwa kujenga mfumo wa e-CMS kwa kuwa haki itapatikana kwa wakati kwa watu wote bila kujali mahali alipo kwa kutumia TEHAMA na kwa kuzingatia ofisi yetu ni mdau muhimu," alisema Mulwambo.

Aliwataka washiriki hao kuzingatia mafunzo hayo ili waweze kutumia ujuzi watakaoupata na kuyafanyia kazi kwa kuzingatia uadilifu na usiri katika utendaji kazi kwa kuwa Mashala ya Sheria ni Ofisi nyeti katika kutunza nyaraka za serikali.

Naye Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mashala ya Sheria wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Dennice Leonard, alisema mfumo huo utawawezesha wananchi kupata taarifa na kufuatilia mwenendo wa mashauri mahakamani kwa kupata ujumbe kwenye simu zao za mkononi na barua pepe.

# Jaji Mkuu: Sheria zetu zina kona nyingi

**Na Grace Gurisha**

"KUNA tatizo kubwa katika mifumo ya sheria ambayo ina kona nyingi zinazotoa fursa kwa mashauri ambayo yamefika mwisho, kurudi tena mahakamani na kuanza upya na kwa bahati mbaya taaluma yetu ya sheria imejengwa kupitia hizo kona."

Hiyo ni kauli ya Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma aliyoitoa juzi jijini Dar es Salaam wakati wa sherehe za utoaji tuzo kwa wadau wa usuluhishi zilizoandaliwa na Mahakama Kuu Kituo cha Usuluhishi, akiwataka wadau wa mahakama wajikite kwenye usuluhishi.

Alisema moja ya maboresho katika karne ya 21 ni usuluhishi, akifafanua kuwa taratibu zao za mahakama na sheria za mwenendo wa madai na jinai, zote zinategemea sheria zilizotungwa katika maudhui ya karne ya 18 na 19.

"Kuna wakati fulani alikuja mgeni kutoka Marekani. Aliposoma sheria yetu ya madai aliandika kwa kusema kwamba sheria zetu ni za zamani na zina 'konakona' nyingi sana, zinaweka fursa za mapingamizi," alisema Prof. Juma.

Jaji Mkuu alisema kuwa wakati wanazungumzia usuluhishi, wasisahau kuangalia sheria zote, waangalie kama kuna haja mgogoro wa ardhi uanzie ngazi ya kata, Baraza la Ardhi, kisha kesi iende tena Mahakama Kuu ambako kuna mapingamzi mengi na kisha iende Mahakama ya Rufani.

"Halafu hapo iwe nchi yenye sheria ambayo ni shindani kibiashara na uwekezaji. Kwa hiyo, kuna tatizo kubwa sana katika mifumo yetu ya sheria. ina kona nyingi.

"Ndiyo maana mawakili watakwambia 'hapo ndipo tunapata chakula chetu, bila hizo kona hatuwezi kusonga'. Kwahiyo, ule ucheleweshaji kwa wengine ni faida ya kupata kipato, kuna haja ya kuangalia sheria zetu upya kabisa," alisisitiza.

Alisema kuwa wapo watu wamediliki kusema kuwa hata shule ya sheria, mfumo wa sheria umejengwa katika maudhui ya karne ya 18 hadi 19 na ndio maana wanapata shida katika teknolojia.

"Tuangalie usuluhishi na taratibu za mahakama zetu. Je, ni ushindani? Taratibu hizo zinaweka mashauri mahakamani zaidi ya miaka mitano hadi sita, mfano Mahakama ya Rufani imeanza kujitahidi kupunguza muda wa shauri lililosajiliwa liondoke si zaidi ya miaka miwili, kuna baadhi ya wateja wanalalamika tunakwenda kasi sana," alisema.

Jaji Mfawidhi wa Kituo hicho, Zahara Maluma alisema ibara ya 107 ya Katiba ya Tanzania inaeleza matumizi ya usuluhishi katika utatuzi wa migogoro huku akizitaja Singapore, Ghana, Marekani na Indonesia kuwa ni baadhi ya nchi zilizofanikiwa katika utatuzi wa migogoro kwa njia hiyo kwa asilimia 90 ya mashauri yanayosajiliwa.

Alisema kuwa mwaka 2023, kituo hicho kilifanya tathmini kuhusu matumizi ya usuluhishi na kubaini kuwa bado migogoro inayohusisha taasisi za kiserikali, taasisi za kifedha na kampuni, huwa hayafanikiwi kirahisi kupitia njia ya upatanishi licha ya kuwa na idadi ndogo kulinganisha na migogoro ya ardhi.

Jaji Maluma alisema hali ya usuluhishi imeongezeka. Mahakama Kuu ikijumuisha Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara, Mahakama za Hakimu Mkazi na Wilaya hadi kufikia Septemba mwaka jana, mashauri 1,532 yalipitia upatanishi. Kati yake, 671 yalitatuliwa kwa upatanishi, sawa na asilimia 44.

"Hii ni mara mbili ya kiwango cha mwaka 2022, ambapo asilimia ya kiwango cha mashauri yaliyotatuliwa kwa njia ya upatanishi yalikuwa asilimia 21," alisema.

Alieleza kuwa Mahakama Kuu Kituo cha Usuluhishi wamefanikiwa kutatua mashauri 84 kati ya 397 yaliyofunguliwa mwaka 2023, huku mashauri 65 kati ya hayo yakihusu migogoro ya taasisi za fedha ikiwamo mikopo yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 666, mashauri 30 yaliyohusu madai ya mikataba huku muda wa usuluhishi ukiwa kati ya siku moja hadi 23.

Miongoni mwa waliopata tuzo hizo ni majaji wastaafu, majaji walio kazini, mahakimu, mawakili wa serikali, mawakili wa kujitegemea, kampuni, Benki ya NMB, ABC, Baraza la Usuluhishi Kata ya Chanika na Twangoma.



Mkurugenzi wa Shirika la Akili Platform Tanzania (APT), Roghat Robert (wa pili kulia), akitoa maelezo ya jinsi ya kutunza mazingira kabla ya kuupanda mche wa mti katika eneo la Shule ya Sekondari Kariakoo, mjini Tabora juzi. Jumla ya miti 500, ilipandwa shuleni hapo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Othman aitaka serikali inusuru wananchi kuuawa na wanyama

**Na Mwandishi Wetu,** TUNDURU

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha ACT- Wazalendo Zanzibar, Othman Masoud Othman, ameitaka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuchukua hatua za haraka kunusuru maisha ya wananchi wa Ruvuma, hasa wilayani Tunduru kuawa na tembo.

Amesema wanyamapori hao wanatoka katika mbuga mkoani Ruvuma na kuvamia maeneo ya vijiji vilivyo karibu na mbuga za mkoa huo.

Othman ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, aliyasema hayo jana alipowasalimia wananchi wa vijiji vya Mtima na Lukubula wilayani Tunduru na wananchi kulalamika kwamba watu zaidi ya 50 tayari wameuawa na tembo na serikali haijachukua hatua za kudhibiti madhara ya wanyama hao.

Alisema suala hilo lina madhara makubwa kwa wananchi hao na taifa kwa jumla, hivyo serikali inapaswa kuchuka hatua.

Othman alisema thamani ya mwanadamu ni kubwa zaidi, ndio maana sheria zinaamuru aliyeua auawe akithibitika. Hivyo, tembo wanaoua watu, serikali inapaswa kuchukua hatua za kunusuru maisha ya watu.

Alisema wanyama hao ni muhimu kwa uchumi lakini wananchi ndio wapigakura wanaowaweka viongozi kisheria, hivyo wanapaswa kunusuriwa na madhara yanayotokana na wanyama hao.

Alisema kuwa hiyo ni kero kubwa kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na chama chao kimejipambanua kutetea haki za wananchi, hivyo kero zao ataziwasilisha katika mamlaka husika ili serikali iuchuke hatua za haraka.

Aliwataka wananchi kuendelea kukiunga mkono chama chake cha ACT ili kiwe na uwezo zaidi wa kuwatetea wananchi kama kilivyojimbanua katika sera zake za kujenga Tanzania moja kwa manufaa ya wote.

Othman yuko Tanzania Bara kwa ziara maalum ya kichama katika mikoa ya kusini mwa Tanzania. Tayari ameshawasili Mtwara kuendelea na ziara ya kichama katika mkoa huo.

# Wapandishwa kizimbani kwa mashtaka kuhujumu mbolea

**Na Moses Ng'wat,** SONGWE

MFANYABIASHARA maarufu wa pembejeo za kilimo Mkoa wa Songwe, William Lema na wenzake watatu, wamefikishwa katika mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Songwe, wakikabiliwa na mashtaka 10, yakiwamo ya uhujumu uchumi na utakatishaji fedha.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo namba 1211 ya mwaka 2024 ni Omary Hashimu, ambaye alikuwa mwajiriwa wa muda wa kampuni ya mawasiliano ya simu za mkononi ya Vodacom Tanzania, Camilius Honde ambaye ni mshtakiwa namba tatu akiwa kama wakala wa kampuni ya mawasiliano ya Tigo na Robert Mrema ambaye ni mshtakiwa namba nne.

Mshtakiwa wa kwanza, Lema, hakuhudhuria mahakamani, wakili wake Isaya Mwanri akidai kuwa mteja wake asingeweza kufika kutokana na kuugua na kulazwa hospitalini.

Akisoma hati ya mashtaka mahakamani huko juzi, Wakili wa Serikali Mkoa wa Songwe, Joseph Mwakasege mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Hassan Makube, alidai katika eneo la Mlowo, wilayani Mbozi, msimu wa kilimo wa 2022/23 na 2023/24, washtakiwa waliongoza genge la uhalifu na kujinufaisha.

Katika shtaka la pili linalowakabili mshtakiwa wa kwanza na wa pili (Lema na Hashimu), wanadaiwa kuingilia mfumo wa mbolea ya ruzuku na kusababishia serikali hasara ya Sh. bilioni 1.86.

Wakili wa Serikali Mwakasege alidai mahakamani huko kuwa, vitendo vya washtakiwa hao kuingilia mfumo wa serikali wa ruzuku ya mbolea, kilisababisha wajinufaishe na kujipatia mifuko ya mbolea ya ruzuku 1,793 iliyokutwa kwenye ghala la mshtakiwa wa kwanza, Lema.

Washtakiwa hao wanadaiwa kukwepa kodi katika Mamlaka ya Mapato (TRA), ikiambatana na mashtaka mengine ya kushindwa kutoa risiti za kielektroniki ili kuhalalisha biashara yao.

Katika shtaka la sita, lililowakabili washtakiwa wa pili na wa tatu (Hashimu na Honde) linahusu kuingilia mfumo wa mawasiliano kinyume cha Sheria ya Makosa ya Kimtandao Na. 14 ya mwaka 2015, huku shtaka la saba ni kuingilia mawasiliano ya simu ya mtu mwingine kwa lengo la kurahisisha kutenda uovu wao.

Wakili Mwakasege alidai kuwa shtaka la nane linamkabili mshtakiwa wa tatu, Honde. Akiwa wakala wa kusajili laini za simu katika kampuni ya mawasiliano ya simu ya Tigo, licha ya kampuni hiyo kufunga mfumo wa kusajili wakulima, aliendelea kubaki kwenye mfumo na kuendelea kuingiza wakulima katika mfumo huo kinyume cha sheria.

Pia mshtakiwa huyo anadaiwa kutoa taarifa za uongo kwenye mfumo wa ruzuku ya mbolea, akidanganya kuwa ana mashamba na kunufaika kwa kujipatia mifuko 5,000 ya mbolea ya ruzuku.

Shtaka la 10 linawakabili washtakiwa wote wanne. Wanadaiwa kutakatisha Sh. milioni 373 baada ya kufanya miamala ya Sh. milioni 455 na kulipa kodi TRA Sh. milioni 81.

Washtakiwa hawakuruhusiwa kujibu chochote huko kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi. Kesi hiyo iliahirishwa hadi Januari 30, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa. Washtakiwa waliokuwapo mahakamani walirejeshwa mahabusu.

Wakili wa washtakiwa namba moja na nne (Lema na Mrema), Mwanri, aliomba upelelezi wa kesi hiyo uharakishwe kwa kuwa wateja wake wameshtakiwa kwa makosa yasiyodhaminika.





# Manyara kuzalisha tani 1.9 za mazao

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MKOA wa Manyara unatarajia kuzalisha tani 1, 934,000 za mazao ya chakula na biashara katika msimu ujao wa mavuno kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya mbolea na kuzalisha kwa tija.

Hayo yalisemwa na Ofisa Kilimo wa Mkoa huo, Samweli Dahaye jana wakati wa mahojiano maalumu na Nipashe juu ya msimu huo wa kilimo.

Dahaye alisema katika msimu huo mkoa huo unatarajia kulima hekta 516,000 za mazao ya chakula na kuzalisha tani milioni 1.26 na ya biashara hekta 336,000 tani 6,74,000.

Alisema wataongeza matumizi ya mbolea ili wakulima waweze kuzalisha mazao yao ya chakula na biashara kwa tija.

Kwa msimu wa kilimo uliopita, Manyara ulizalisha tani 521,259 za mazao ya chakula na kuwa na ziada ya tani 67.

Katika msimu huo, hali ya ukame ilijitokeza katika wilaya za Simanjiro na Babati kutokana na kuathirika na ukame.

Meneja wa Chama cha Kilimo na Masoko cha Gallapo (AMCOS), Lohay Langay alisema licha ya hali ya hewa kuwa nzuri kwa kilimo, upatikanaji wa mbegu ni mgumu.

Lohay alisema kuna baadhi ya mazao mbegu hazipatikani na zinazopatikana bei yake iko juu.

Aliiomba serikali kusaidia uhakika wa upatikanaji wa mbegu bora ili wakulima waweze kuzalisha kwa tija.

Meneja huyo aliomba serikali kuzisimamia Mamlaka zinazohusika na kuzalisha mbegu kuhakikisha wanazalisha mbegu bora ambazo zitakidhi vigezo ili zisiwasababishie hasara wakulima.

# Ukaaji kama chura, kobe majanga

**Na Oscar Assenga,** TANGA

DAKTARI Bingwa wa Mifupa wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga (Bombo), Dk. Said Nondo, amesema chanzo cha matatizo ya watu kuugua mgongo ni ukaaji mbaya kama chura na kobe kwa muda mrefu.

Dk. Nondo aliyasema hayo jana wakati akitoa elimu kuhusu maumivu ya mgongo yanayotokana na ukaaji mbaya kwa muda mrefu.

Alisema matatizo hayo huwakumba watu mbalimbali wakiwamo watoto wa shule, wafanyakazi ofisini na viwandani.

Alisema kama wanafanyakazi kwa saa tano au sita wakiwa wamekaa, wanapaswa kusimamama kila baada ya saa tatu ili kunyoosha misuli.

"Unapokaa muda mrefu bila kuinuka unasababisha misuli kuanza kubana taratibu. Ukaaji uliosalama na uliobora ni ambao unaliwezesha umbo la ute wa mgongo kuendelea kuwa kwenye hali yake ya uhalisia ya wima bila kupinda mgongo kuelekea mbele," alisema Dk. Nondo na kuongeza kuwa:

"Unapokaa wima unaupa urahisi ute wa mgongo kuendelea kubaki kwenye hali yake ya uhalisia na kwa watu wa ofisini kuna viti maalumu ambavyo mbele yake kumetengenezwa umbo maalumu ambalo linasaidia kukaa katika hali iliyosalama zaidi."

Aliendelea kusema kuwa kukaa kwa kutoa mgongo kama chura au kobe kunasababisha misuli ya mgongo kutoka kwenye kisogo mpaka kwenye kiuno kukaza taratibu kisha kuleta maumivu makali.


Dk. Nondo, alisema endapo maumivu machache ya mara kwa mara yataendelea kwa muda mrefu, yatasababisha umbile la mgongo kubadilika kutoka kwenye la asili la C na kunyooka na kuwa kama rula, kuminya pingili laini, kutanuka, kuminya misuli ya fahamu inayopasuka kwenye miguu.

Alisema misuli hiyo inatoka kwenye matundu madogo kati ya pingili moja na nyingine ikipitia kwenye makalio, nyuma ya paja na kushuka kwenye miguu.

Alisema hali hiyo inaweza kusababisha maumivu kushuka kutoka kwenye kiuno, makalio, miguu na inapozidi kwa muda mrefu inaambatana na ganzi, miguu kuwaka moto, kukosa nguvu au kukaza hasa usiku.

"Ni sababu moja inayoongoza kuleta maumivu ya mgongo kwenye rika zote kawaida ni umbile la mgongo halikuumbwa lenye kunyooka bali limeumbwa likiwa na mipindo mitatu, mifupa ya mgongo ambayo unaweza kugawa maeneo matatu la kwanza ni shingo, kifuani kuna upinde unaangalia mbele na chini kuna S inaangalia chini sasa katika ukaaji watu wengi wanakaa kwa kuinua mgongo lakini kifua chake kinakuwa kimekwenda mbele," alisema.

Dk. Nondo alitoa ushauri ili kuzuia matatizo ya mgongo, maumivu ambayo yanatokana na ukaaji mbaya ni watu kuzingatia ukaaji salama ambao haupindishi mgongo ili kuweka ute wa mgongo kwenye umbo lake asili.



Askari wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, wakitoa elimu kwa abiria wa basi kuhusu umuhimu wa kujua haki zao, ikiwamo kutoa taarifa wanapoona kuna viashiria vinavyoweza kusababisha ajali jijini Arusha jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Masoko ya halmashauri yakatiwa maji

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAFANYABIASHARA wa baadhi ya masoko jijini hapa, wapo hatarini kukumbwa na magonjwa ya mlipuko kutokana na Halmashauri ya Jiji la Arusha kushindwa kulipa ankara za maji.

Licha ya changamoto ya maji kwenye masoko hayo, pia wamelalamikia miundombinu mibovu ya masoko, ikiwamo baadhi kutokuwa na mapipa ya kuhifadhia taka, vyoo na huduma ya majisafi.

Akizungumza katika kikao kazi kilichoongozwa na Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Arusha, Timoth Sanga, kwa lengo la kusikiliza kero zinazowakabili wafanyabiashara katika masoko yanayomilikiwa halmashauri hiyo, Katibu wa Soko la Giriki, Ommary Salim alisema wamekatiwa maji kutokana uongozi wa Jiji kutolipa ankara za maji kwa wakati.

"Hali ni mbaya katika Soko la Giriki, hakuna maji kwenye vyoo wala maji ya huduma nyingine. Wafanyabiashara tunachota maji Mto Kilombero kwa ajili ya kutumia, tunaomba uongozi wa CCM wilaya utusaidie halmashauri ilipie maji kwa sababu inakusanya ushuru mkubwa katika soko hilo," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa Soko la Mbauda, Elizabeth Ayubu, alisema wafanyabiashara wanalazimika kupanga bidhaa zao chini kutokana na halmashauri hiyo kutowaweka miundombinu na kusababisha tope kujaa.

"Tuko hatarini kupata magonjwa ya mlipuko soko halina maji, vyoo ni vichafu halmashauri haileti vifaa vya usafi, hakuna mapipa ya taka, taka zimejaa hapa hazichukuliwi kwa wakati Jiji linakusanya ushuru kila siku hadi siku za sikukuu na Jumapili.

"Tukiuliza kwanini viongozi wanatuambia tusubiri mradi wa kuboresha miji na majiji nchini unaotarajiwa kutekelezwa na Benki ya Dunia wakati hatujawahi hata kuona mchoro, tunaomba CCM mtusaidie ni changamoto ya muda mrefu," alisema.


Mwenyekiti wa Soko la Samunge Njola Mitaji, alisema wanaomba soko hilo lijengwe upya kwani tangu lilipoungua serikali haikujenga badala yake wafanyabiashara wamejijengea vibanda vya muda na kwamba wanakabiliwa na changamoto ya upungufu wa vyoo.

"Changamoto kubwa ni vibaka wanaibia hadi raia wa kigeni wanapopita jirani na soko letu na kukimbilia kwenye jengo chakavu la serikali wanakovutia bangi na kucheza kamari na wakikamatwa na polisi baada ya muda mfupi wanarejea mtaani," alisema.

Akijibu changamoto hizo, Mwanasheria wa halmashauri hiyo, Idd Ndabhona alisema wanazifanyia kazi, ikiwamo kumwaga moramu kwenye masoko kutokana na kuharibiwa na mvua na mengine yapo kwenye bajeti kwa ajili ya ukarabati.

Kuhusu Soko la Giriki ambalo limekatiwa maji na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jiji la Arusha (AUWSA), Ndabhona aliahidi kuwa ndani ya siku mbili watarejesha huduma hiyo.

Akizungumza baada ya kupokea malalamiko hayo, Sanga aliwataka viongozi wa masoko walioajiriwa na halmashauri hiyo kusimamia majukumu yao kikamilifu na kuwasilisha kwa Mkurugenzi wa Jiji kwa wakati changamoto zinazowakabili wafanya biashara hao.



## HABARI KANDA YA ZIWA

# Kipindupindu chatikisa jijini Mwanza

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

MAAMBUKIZI ya kipindupindu mkoani Mwanza yameongezeka kutoka watu 34 hadi kufikia 80 katika kipindi cha wiki moja huku hali ikitajwa kuwa mbaya kutokana na kutikisa zaidi maeneo ya katikati ya Jiji la Mwanza.

Takwimu hizo zilitolewa juzi na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Dk. Thomas Rutachunzibwa, baada ya semina ya kuwajengea uwezo waandishi wa habari mkoani hapa kuhusu ugonjwa huo. Dk.Rutachunzibwa alisema kuna haja ya kuongeza nguvu zaidi kuelimisha jamii kuzingatia maelekezo ya kitabibu ili kukabiliana na ugonjwa huo.

"Ugonjwa huu ukimkuta mtu ndani ya nusu saa anabadilika na kuwa mtu mwingine na hii ni kutokana na kuharisha na kutapika mfululizo hali inayosababisha mgonjwa akose nguvu, hivyo inatakiwa awahi katika kituo cha kutolea huduma za afya," alisema Dk. Rutachunzibwa.

Licha ya kutaja vituo maalumu vilivyotengwa na serikali mkoani hapa kuwahudumia wagonjwa hao vya afya vya Mkuyuni na Buzuruga aliwataka wananchi kufika katika kituo kilichopo karibu nao ili wahudumiwe haraka na kuokoa maisha yao.

Baadhi ya waandishi wa habari waliishauri serikali kuhakikisha inatimiza wajibu kudhibiti vyanzo vya ugonjwa huo na uchafu uliokithiri katikati ya jiji hilo.

"Yapo maeneo yenye uchafu uliotelekezwa, chemba za vyoo zinazomwagwa majitaka katika makazi ya watu hali ambayo imekuwa ikitajwa kueneza kwa kasi ugonjwa huu, hivyo mkidhibiti haya mambo tunaimani ugonjwa huu utakuwa historia," alisema Welington Masele.

Kuhusu uchafu uliokithiri katika jiji, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Dk. Rutachunzibwa, alisema serikali imechukua hatua za haraka kudhibiti kwa kushirikiana na mamlaka.

Mratibu wa Elimu ya Afya kwa Umma Mkoa wa Mwanza, Renard Mlyakado alisema dalili za ugonjwa huo huanza kuonekana ndani ya saa 24 hadi siku tano baada ya maambukizi.

Mlyakado alizitaja dalili hizo kuwa ni kuhara kinyesi kinachofanana na maji ya mchele, kutapika, mwili kulegea na kukosa nguvu, maumivu ya misuli, upungufu wa maji mwilini, ngozi kusinyaa, midomo kukauka na macho kudumbukia ndani.

Aliihimiza jamii kutumia vyakula vya moto, kuosha kwa maji safi vyakula vinavyoliwa bila kupikwa kama matunda, mbogamboga, kusafisha vyombo kwa maji ya moto, kuepuka uchafuzi wa vyanzo vya maji.

"Jamii itambue ugonjwa huo ni rahisi kuambukiza, ni rahisi kujikinga na ni rahisi kupoteza maisha," alisema.



Diwani wa Kata ya Nyakatende, Musoma Vijijini, mkoani Mara, Kisha Marere, akizungumza kwenye mkutano wa kuhamasisha wananchi kuchangia ujenzi wa shule shikizi (awali), katika kijiji cha Kamguruki juzi, ili kuwapunguzia watoto kutembea umbali mrefu kufuata elimu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SHIREMA yapiga marufuku uchimbaji maeneo hatarishi

**Na Mohab Dominick,**
KAHAMA

CHAMA cha Wachimbaji Wadogo Mkoa wa Shinyang (SHIREMA) kimepiga marufuku uchimbaji madini katika maeneo hatarishi ili kuepuka maafa.

Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa Nchini (TMA) na Tume ya Madini, ilitoa tahadhari kwa wachimbaji wadogo katika kipindi hiki mvua zinaendelea kunyesha kuwa waangalifu na kufunga uchimbaji madini katika maeneo hatarishi.

Mwenyekiti wa SHIREMA, Hamza Tandiko, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu chama hicho kulivyojipanga kukabiliana na majanga katika kipindi hiki ambao mvua zinazoendelea kunyesha nchini.

Tandiko alisema kama waangalizi wa wachimbaji, wamepewa maagizo na mamlaka husika kuchukua tahadhari ili kunusuru maisha ya wachimbaji wadogo na kuboresha miundombinu katika maeneo yenye majimaji.

Alisema wanatoa elimu ya kujikinga na majanga mahali pa kazi huku akiwataka wachimbaji hao kuhakikisha wanazingatia maagizo ya serikali.

Ofisa Madini Mkoa wa Kimadini wa Kahama, Joseph Kumbulu, alisema wametoa matangazo katika maeneo yote ya uchimbaji ili kuhakikisha yapo salama.

**Ofisa Madini Mkoa wa Kimadini wa Kahama, Joseph Kumbulu, alisema wametoa matangazo katika maeneo yote ya uchimbaji ili kuhakikisha yapo salama.**

Kumbulu alisema hawatapenda kuona maeneo hatarishi yanaachwa kufanyiwa kazi haraka ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea.

Alitoa wito kwa wachimbaji kuhakikisha hayatokei madhara yoyote kwa kipindi hiki na kuonya kuwa hawatasita kufunga mgodi utakaobainika kuleta madhara kwa wachimbaji.

## Polisi, wanahabari waafikiana

**Na Timothy Itembe,**
MARA

JESHI la Polisi Mkoa wa Kipolisi Tarime/Rorya na waandishi wa habari mkoani hapa wameafikiana kutekeleza majukumu yao pamoja ili kuepuka migongano baina yao.

Pande hizo mbili zilifikia makubaliano hayo juzi katika majumuisho ya midahalo baina ya Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Mara (MRPC) na Polisi Mkoa wa Mara na Mkoa wa Kipolisi Tarime/Rorya ulioratibiwa na Muungano wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC).

Kamanda wa Polisi Tarime /Rorya, Mark Njera, alisema wanatakiwa kutekeleza majukumu kwa kufuata weledi, kanuni, sheria na taratibu ili kulinda na kudumisha amani ya nchi.

Njera alisema jeshi hilo liko tayari kufanya kazi bega kwa bega na wanahabari kwa manufaa ya jamii.

Makamu Mwenyekiti wa MRPC, Raphael Okelo, alisema kupitia mijadala iliyoibuliwa na kuridhiana, watahakikisha wanaimarisha uhusiano baina yao.

Okelo alisema midahalo hiyo ni matokeo ya tafiti zilizofanywa na taasisi za habari na kubaini kulegalega mahusiano kwa pande hizo.

Makamu Rais wa UTPC, Pendo Mwakembe, alisema ili kuimarisha uhusiano mpya na maazimio kutekelezwa, wameamua kuunda kamati za uratibu wa kazi za waandishi wa habari na askari kutoka kwa makamanda wa jeshi hilo ili kuwaweka pamoja.

ama
ALHAMISI JANUARI 18, 2024
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

Zanzibar ilivyopiga hatua maendeleo sekta ya afya



Ukurasa 14

**Marufuku kula nyama ya mbwa, yawa ajenda nzito hadi wasomi**

RIPOTI KILICHOTWALIWA SEKTA YA AFYA 2023

# Waziri Ummy: Ubunifu Awamu VI, Utalii Tiba tumevuna wageni 6931

• Aorodhesha malengo manne 2024

**Na Yasmine Protace**

KATIKA kuhakikisha wananchi nchini wanapata huduma bora za afya, serikali imezungumzia mafanikio katika sekta hiyo kwa mwaka jana na iendako mwaka huu.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akatafsiri iliyoko mwaka huu inagusa vipaumbele vinne, ikiwa ni sehemu ya uwasilisho wa utoaji huduma za afya nchini, unavyoendelea akirejea kilichotendeka mwaka jana na kinachofuata mwaka huu.

Vilevile, Ummy anafafanua kilichotekelezwa kimataifa mwaka jana, kuwapo wagonjwa 6,931 kutoka nje ya nchi walitibiwa nchini katika hospitali sita tofauti.

Ummy anataja mwaka juzi, idadi ya wagonjwa hao kutoka nje ya nchi waliofika Tanzania kutibiwa walikuwa 5,705, hivyo imefanya ongezeko hilo kufika asilimia 121.

Waziri anaisifu serikali awamu ya sita kwa uwekezaji mkubwa iliofanya, akimtaja Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kufanya maboresho katika huduma za kibingwa na ubobezi sekta ya afya, hata ikasaidia kuvutia wagonjwa nchi jirani kufuata huduma za afya.

Ukiwa unaitwa Utalii Tiba, Waziri Ummy alisema wagonjwa wake wanatoka nchi jirani za Comoro, Malawi, Burundi, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasi Congo (DRC), Uganda, Zimbabwe na Kenya.

Hapo anavitaja vituo vya matibabu hayo viko sita, ambazo ni: Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH); Taasisi ya Saratani ya Ocean Road; Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete; Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI); Hospitali ya Aga Khan na Hospitali ya Saifee.

Waziri anataja jumla ya wagonjwa 15,386 wamepatiwa huduma mpya za 'CT-SCAN' mwaka jana, katika hospitali za rufani za mikoa, ambazo zilikuwa hazipatikani mahali hapo.



*Wazazi wakishiriki huduma za kliniki wilayani Meru. **PICHA: MTANDAO.**

"Uwekezaji huu umeleta mabadiliko makubwa katika huduma za uchunguzi wa magonjwa na hivyo huduma hizi kuwafikia wananchi kwa urahisi katika maeneo wanayoishi na kupunguza usumbufu wa kupoteza muda na gharama za kupata matibabu,"anasema.

**SURA YA MAFANIKIO**

Waziri anafafanua kuwapo mashine za kuchunguza magonjwa kama ya misuli, mishipa ya damu na fahamu, ubongo na uvimbe (MRI) zimeongezeka kufika 13, wakati mwaka mmoja nyuma 2022, zilkuwapo sita pekee.

"Pia, mashine ya kuchunguza magonjwa ya misuli, ubongo, viungo vya mwili (CT SCAN) zimeongezeka kufikia 45 mwaka 2023 ambapo ilikuwa 22 tu," anasema.

Anaongeza kuwa, kuna mashine za 'Digital X- Ray' zimeongezeka kufikia 346, zote sasa zinafanya kazi, ilhali mwaka 2022 zilikuwa 296 pekee.

Zingine anazitaja ni mashine za 'Utra Sound', ambazo Desemba 2022 zilikuwa 192, lakini baada ya mwaka mmoja, kwa maana hadi mwezi uliopita, idadi ni 512, kwa maana ziada ya mashine 320 ndani ya mwaka.

Mengine anayoyataja waziri, ni idadi ya vitanda vya wagonjwa katika kipindi cha mwaka 2023 vimeongezeka kufika 126,209 kutoka 104,687 mwaka 2022; ongezeko la vitanda 21,522.

"Kwa kuzingatia idadi ya watu wa Tanzania Bara, uwiano wa vitanda kwa idadi ya watu ni sawa na vitanda 2.1 kwa kila watu 1000, viwango vya WHO kwa kila watu 1000 ni uwiano wa vitanda 2.5.

Ummy anasema, kuongezeka vitanda vya wagonjwa kumesaidia tija ya huduma za afya, hususani afya ya uzazi, mama na mtoto.

Waziri anafafanua kwamba, mnamo Desemba 2022 kulikuwapo vitanda vya wagonjwa mahututi (ICU) 528, lakini ndani ya mwaka mmoja, Desemba 2023, idadi ikaongezeka kufika vitanda vya ICU 1,000, wastani unaokaribia mara mbili.

"Wagonjwa wanaohitaji huduma za uangalizi maalumu (ICU) kwa sasa wanapata huduma hiyo kwa urahisi, ukilinganisha na miaka ya nyuma," anaongeza Ummy.

Anaeleza ongezeko la vitanda vya ICU katika hospitali za umma, inalenga kuboresha hu-

Inaendelea Uk. 13

AFYA

# Zanzibar ilivyopiga hatua maendeleo sekta ya afya

**Na Mwandishi Wetu**

AFYA ni msingi mkuu wa maendeleo endelevu katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Ni dhahiri kwamba bila jamii kuwa na afya bora hakuna maendeleo ya aina yoyote.

Zanzibar leo ikiwa inatimiza miaka 60 ya Mapinduzi ya mwaka 1964, moja ya mambo ya kujivunia katika kipindi hicho ni maendeleo katika sekta ya afya. Yako mambo mengi ya kujivunia katika sekta hiyo na hata kuigwa na watu wengine kutokana na kile Zanzibar ilichokifanya katika afya ndani ya miaka 60 ya Mapinduzi.

Akizungumzia maendeleo na mafanikio ya sekta ya afya katika miaka 60 ya Mapinduzi hivi karibuni, Waziri wa Afya wa Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, anasema dhamira ya kuhakikisha wananchi wa Zanzibar wanakuwa na uhakika wa afya bora ikiwamo kupata matibabu bure, ina historia ndefu tangu wakati wa harakati za kupigania uhuru wa visiwa hivyo.

"Historia hii inaanzia wakati wa harakati za kujikomboa kutoka utawala wa kikoloni. Chama cha Afro Shiraz (ASP) katika manifesto (ilani) yake ilikuwa ikijinadi kwamba ikishinda afya na elimu vitakuwa bure kwa wananchi wa Zanzibar.

"Watu wengi walikuwa wa kipato cha chini, hivyo wasingeweza kupata matibabu sahihi. Baada ya Mapinduzi, Sheikh Abeid Amani Karume (Rais wa Kwanza wa Zanzibar) alitangaza kuwa matibabu ni bure. Alipiga marufuku hospitali binafsi na zikafungwa, wamiliki wakaondoka," anasema.

Kutokana na hali hiyo, kwa mujibu wa Mazrui, tangu wakati huo tegemeo kubwa katika matibabu lilikuwa serikali ambayo ilitoa dawa, vifaa tiba, matibabu bure, madaktari na wauguzi.

"Tukirudi nyuma kidogo, kabla ya Mapinduzi, Karume alikuwa Waziri wa Afya na baada ya Mapinduzi, Aboud Jumbe (Rais wa pili wa Zanzibar) alikuwa Waziri wa Afya. Sera ya Afya ilianzishwa na ikapelekwa Baraza la Mapinduzi na kila baada ya miaka 10 ilikuwa ikifanyiwa marejeo hadi sasa mimi nikiwa waziri," anabainisha.



Hospitali mpya ya Lumumba, iliyoko Zanzibar. **PICHA: MAKTABA**

> Watu wengi walikuwa wa kipato cha chini, hivyo wasingeweza kupata matibabu sahihi. Baada ya Mapinduzi, Sheikh Abeid Amani Karume (Rais wa Kwanza wa Zanzibar) alitangaza kuwa matibabu ni bure.

### KABLA YA MAPINDUZI

Waziri Mazrui anasema huduma za afya Zanzibar zilianza mwaka 1884 baada ya ujio wa wakoloni ilipojengwa hospitali ya misheni kwa ajili ya kutibu wazee na watoto waliokuwa katika hali mbaya karibu na kufa.

Baada ya hapo, anasema mwaka 1890, mfanyabiashara Sewa Haji alijenga hospitali katika jengo kongwe kwenye Hospitali ya Kuu ya Mnazi Mmoja kabla ya Muhimbili, Dar es Saaam kwa gharama ya Rupee za India 3,000 kwa wakati huo.

Kwa mujibu wa Mazrui, kabla ya Mapinduzi, hali ya huduma za afya ilikuwa duni na vifo vilikuwa vingi hasa kwa watoto. Anatoa mfano wa mwaka 1919 walipofariki watoto 400 hadi 500 kati ya 1,000 hali ambayo ilisababisha kuanzishwa kwa Chama cha Wakunga Zanzibar (ZMA). Chama hicho kilikuwa na lengo la kupunguza vifo vya uzazi hasa maeneo ya vijijini ambako vilikuwa vingi.

Pia anasema kulikuwa na ushajihishaji wa ujenzi wa vituo vya afya ili kuwezesha wananchi kupata matibabu. Mwaka 1907 wakati wa utawala wa Sultan, anasema vilijengwa vituo vya afya vya serikali vilijengwa Makundichi na Mkokotoni vyenye uwezo wa kulaza wagonjwa 10 hadi 15 kwa wakati mmoja.

Uingereza ilipochukua madaraka, anasema ilijenga hospitali nne ambazo kwa kiasi kikubwa zilisaidia kwa kiasi fulani kupunguza changamoto za ukosefu wa huduma za afya. Hata hivyo, anasema kulikuwa na uhaba wa wafanyakazi, hivyo yaliandaliwa mafunzo ya haraka kwa wahudumu wa afya.

Maendeleo zaidi katika sekta hiyo yalionekana kati ya mwaka 1920 na 1930 baada ya kujengwa vituo 30 vya afya Unguja na Pemba pamoja na kuwapo magari ya wagonjwa.

"Lakini jambo ambalo lina historia kubwa kwa Zanzibar ni kwamba ni nchi ya kwanza Afrika Mashariki kuwa na matibabu ya afya ya akili. Inasemekana mtoto wa Mfalme wa Uingereza alipata tatizo la akili na huduma hiyo ikaanzishwa. Pia kulikuwa na kliniki za meno Zanzibar wakati wa ukoloni," anabainisha Mazrui.

Pia anasema mwaka 1930 hospitali binafsi mbili na vituo vya kutolea huduma za afya vilianzishwa na baada ya hapo viliongezeka zaidi kwa sababu ilionekana soko lilikuwapo kwa watu wenye uwezo kifedha.

Aidha, mwaka 1958 Hospitali ya Karimjee ilijengwa Chake Chake na baadaye zilijengwa hospitali zaidi Chake Chake na Wete muda mfupi kabla ya Mapinbduzi.

### MAENDELEO YA SASA

Mazrui anasema wakati Zanzibar inaadhimisha miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu, kuna hatua kubwa katika maendeleo ya sekta ya afya. Anabainisha kwamba kwa sasa kuna vituo vya kutolea huduma 163 zikiwamo zahanati 129 na vituo vya afya 34.

Katika vituo hivyo, anasema kuna huduma mbalimbali kama vile afya ya mama na mtoto (MCH) ikiwamo kujifungua katika zahanati, vipimo na uchunguzi wa magonjwa. Katika vituo vya afya kuna majengo ya wagonjwa wa nje (OPD), maabara zenye vifaa vya kisasa na huduma za uzazi.

"Kwenye vituo vya afya kuna huduma za uzazi kama huduma za wajawazito, kujifungua na baada ya kujifungua. Vituo vya huduma za afya vinapatikana chini ya kilometa tano na vimeenea sehemu nyingi tofauti na ilivyokuwa kabla ya Mapinduzi," anasisitiza.

### FEDHA ZA UVIKO

Kutokana na athari za UVIKO-19 katika sekta mbalimbali ikiwamo ya afya, Mazrui anasema serikali kupitia ilielekeza nguvu katika ujenzi wa hospitali ngazi ya wilaya katika wilaya 10 za Unguja na Pemba.

Hospitali hizo, anasema kila moja ina uwezo wa kulaza wagonjwa 100 hadi 120 kwa wakati mmoja na zina maabara za kisasa kwa ajili ya uchunguzi wa magonjwa mbalimbali, vyumba viwili vya upasuaji, kimoja kwa ajili ya kinamama ili kupunguza vifo vya uzazi.

"Pia kuna ICU (vyumba vya wagonjwa wa uangalizi maalumu) kwa watoto njiti na wenye uzito mdogo. Pia kuna huduma za mionzi, ultra sound, vipimo vya moyo (ECHO) vyote hivi vya kidijitali. Kuna vyumba vya kuhifadhia maiti na huduma za uchunguzi wa maiti (postmortem).

"Awali kulikuwa na ICU moja yenye vitanda vinane lakini sasa kuna ICU 14 zenye vitanda 80. Mwaka 2021 kulikuwa na vitanda 1,445 sasa kuna vitanda 2,645. Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja pekee ina vitanda 750 na kuna huduma ya mama na mtoto, na matibabu ya macho. Hii ni hatua kubwa sana iliyofikiwa na ya kujivunia ndani ya miaka 60 ya Mapinduzi," anasema.

Licha ya mafanikio hayo, Waziri Mazrui anabainisha kwamba vyumba vya upasuaji vimeongezeka kutoka 11 hadi 35 vikiwamo 13 maalum kwa ajili ya kinamama. Pia kulikuwa na eneo moja la huduma za dharura lakini sasa yako 11.

### MIPANGO YA BAADAYE

Katika kuhakikisha sekta hiyo inaendelea kuleta matokeo chanya kwa maendeleo, Mazrui anasema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imejipanga kufanya mambo makubwa zaidi. Moja ya mipango hiyo, anasema ni kupunguza mrundikano wa wagonjwa Mnazi Mmoja kwa kuziwezesha hospitali za mikoa kuwa za rufani.

Msisitizo mkubwa katika mpango huo, anasema ni kuimarisha afya ya msingi kwa kuhakikisha zahanati zina viwango, vifaa tiba na dawa za kutosha pamoja na rasilimali watu.

INAENDELEA UK. 13

# Waziri Ummy: Ubunifu Awamu VI, Utalii Tiba tumevuna wageni 6931

INATOKA UK.11

duma na kupunguza vifo vinavyotokea hospitalini, katika viwango asilimia 20 hadi 30.

"Mfano katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa, walikuwa na vitanda vinane mwaka 2021, hadi mwaka 2023 vitanda vimeongezeka kufikia 20," anasema.

**VITUO VYA AFYA**

Ummy anataja kuwapo vituo vipya 485 vya afya, vikiongezeka kutoka 8,881 Desemba 2022 na sasa viko 9,366, sawa na ongezeko la asilimia 5.5.

Katika hilo, Ummy anafafanua mgawanyiko ulioko ni kwamba vituo vipya vya kutoa huduma za afya kuna: Zahanati - 7,804 (83.3%), vituo vya afya 1,126 (12.02%); hospitali za halmashauri 171 (1.83%), hospitali zenye hadhi ya wilaya -180 (1.92%).

Zingine ni hospitali za rufani za mikoa 28 (1.3%); hospitali zenye hadhi ya mkoa 34 (0.36%), za rufani kanda ziko, tano (0.05%), zenye hadhi ya kanda 11 (0.12%), hospitali maalum sita (0.06%), Hospitali ya Taifa moja- Muhimbili (0.01%).

"Ongezeko la vituo vya kutoa huduma za afya nchini limetuwezesha kusogeza huduma za afya karibu zaidi na wananchi," anasema.

Kuhusu huduma kwa wajawazito nchini, Ummy anasema kila mwaka wanawake milioni mbili hubeba ujauzito na kuna mwamko mzuri wa kuzingatia mahudhurio kliniki.

Pia, anafafanua huduma ya afya ya uzazi, mama na mtoto ni kati ya yaliyofanyiwa tathmini na Wizara ya Afya mwaka jana, kuashiria viashiria vikuu 16.

Miongoni mwa viashria ni mahudhulio angalau mara nne au zaidi (ANC Visit) kwa kundi hilo" akieleza, kimataifa wajawazito kujifungua vituo vya afya ni kiashiria cha ubora wa afya nchini.

Katika ripoti hiyo ya serikali, mwaka 2023 kuna wajawazito 2,442,580(102%) walihudhuria kliniki mara nne katika kipindi cha ujauzito wao.

"Licha ya kuwa hivyo, bado Tanzania ipo katika lengo lililojiwekea kufikia asilimia 80% mwaka 2020, kama ilivyoelekezwa na Shirika la Afya Duniani (WHO)," inafafanua ripoti, Watanzania wakipongezwa kuwa na mwamko mkubwa wa utekelezaji ajenda hiyo.




Waziri Ummy Mwalimu akizindua kampeni ya chanjo. **PICHA: MTANDAO**

**VIPAUMBELE VIJAVYO**

Taarifa ya serikali inaeleza sekta ya afya, imedhamiria kugusa zaidi ngazi ya msingi kiafya, ikiteua vipaumbele vinne vya mwaka huu, Waziri Ummy akivitaja ni: Kuimarisha afya za kinga; kuwezesha wananchi wajikinge na magonjwa; pia kuwezesha utambuzi mapema wa wagonjwa.

"Kipaumbele hiki kitaangalia kuimarisha huduma za chanjo na lishe hususani kwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano," anasema.

Ligine analitaja, wizara itaanzisha huduma za watumishi wa afya ngazi ya jamii (CHW), huku pia ikiendelea kutoa elimu kwa umma kujikinga na magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza (MYA).

Katika sura ya pili, waziri anaahidi mabadiliko ya mtindo wa maisha kwa jamii, ikiwamo kuzingatia ulaji unaofaa na kufanya mazoezi.

Anaongeza kuwa kipaumbele cha pili ni kuendelea kuimarisha ubora katika vituo vya umma za kutoa huduma za afya katika ngazi zote, zikiwamo zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, halmashauri, hospitali za rufani, mikoa na kanda, hadi hospitali za taifa.

Hapo anataja maeneo maalum kama kuwekeza kwenye miundombinu ya kutoa huduma, kukamilisha ukarabati wa miradi ya ujenzi na huduma za kinga kwa wakati sahihi.

Ni hatua anayoitaja itaendana na maboresho kwenye teknolojia ya mawasiliano ili kuwapunguzia wateja muda wa kusubiri huduma, pia kuimarishwa mawasiliano kati ya kituo kimoja na kingine katika mnyororo wa rufani.

Anataja kipaumbele cha tatu, ni kuongeza idadi ya watumishi wa afya katika ngazi zote sambamba na kuwajengea uwezo watumishi wa afya walio kazini.

"Kwa kuwapeleka madaktari bingwa waliopo Hospitali za Rufani za Mikoa katika vituo vya afya na hospitali za wilaya kutoa mafunzo kwa vitendo (mentorship)," anasema.

Anakitaja kipaumbele kingine ni kutoa huduma bora za afya kwa wajawazito na watoto, kupitia utekelezaji wa kampeni ya madaktari bingwa (Madaktari bingwa wa Mama Samia) hadi katika afya ya ngazi ya msingi.

Waziri Ummy anahitimisha kipaumbele cha nne, kwamba ni kutekeleza Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, inayowawezesha wananchi kupata huduma ya afya bila ya kikwazo cha fedha.

Anaongeza kuwa, hapo kuna kukamilishwa mwongozo wa gharama wa utoaji huduma za afya za umma, ili kuwapo uwiano sawa wa bei.

Hapo waziri ana msisitizo wake, kwamba bei za utoaji za huduma ni kipaumbele kingine, serikali ikijielekeza kuimarisha njia na kupunguza malalamiko yanayohusu matibabu ya makundi maalumu ya wagonjwa, wanaostahili msamaha huo.

Hilo analitaka kuambatana na walio na umri chini ya miaka mitano, wajawazito na wazee wasio na uwezo.

Pia Waziri Ummy akataja maeneo ya kuongezwa uwezo wa ndani kuzalisha vifaa tiba na dawa, kuimarisha usimamizi wenye weledi na maadili kwa wataalamu wa afya nchini.

**CHANGAMOTO ZA 2023**

Ripoti ya Waziri Ummy, inadokeza changamoto sita serikali ilikumbana nazi katika afya mwaka jana.

Hapo anaorodhesha upungufu wa watumishi sekta ya afya; na wakalini katika ubora wa huduma kwa baadhi ya maeneo ya utoaji huduma, kutokana na usimamizi usiofaa kwa baadhi ya watumishi.

Nyingine anaitaja ni mwitikio mdogo kwa wananchi kujiunga na huduma ya bima ya afya, hivyo serikali ilishindwa kugharamia huduma mbalimbali wanazohitaji.

Anataja lingine ni kuongezeka magonjwa yasiyoambukizwa (NDCs), mfano kisukari.

## Zanzibar ilivyopiga hatua maendeleo sekta ya afya

INATOKA UK.12

"Mpango wa sasa wa mwaka 2023 hadi 2025 ni kuhakikisha kila jimbo lina kituo cha afya, hivyo mkakati ni kuwa na vituo vya afya 50 ifikapo muda huo. Pia kuwa na hospitali za mikoa katika kila mkoa. Chake Chake na Wete ujenzi wa hospitali hizi utaanza wakati wowote.

"Hospitali ya Mnazi Mmoja itakuwa hospitali ya kisasa na nusu ya majengo yatavunjwa na kujengwa mpya ili kuifanya kuwa ya rufani kwa Unguja na Pemba. Hospitali ya Bumbwini pia itakuwa ya rufani," anasema.

Waziri pia anabainisha kwamba kumekuwa na ongezeko la watoto wanaozaliwa wakiwa na tatizo la moyo. Kutokana na tatizo hilo, anasema serikali imeamua kujenga hospitali kwa ajili ya matibabu ya maradhi hayo na kwamba eneo limeshatengwa na michoro imeshakamilika kwa ajili ya ujenzi.

Mpango mwingine, anasema ni kuongeza rasilimali watu kwa maana ya madaktari bingwa wabobezi, madaktari bingwa, mdaktari na madaktari wasaidizi, wauguzi, wafamasia na wataalamu wa mionzi na baabara.

"Kufikia mwaka 2027, lengo ni Zanzibar kuwa na rasilimali watu ya kutosha katika afya. Tunataka kupiga hatua kubwa zaidi katika hili. Kabla ya Mapinduzi madaktari na wauguzi walikuwa wazungu na wale wa asili ya kiasia. Waafrika walikuwa wachache, mwaka 1935 alikuwapo mwafrika mmoja tu, Kingwabi Hassan," anasema.

Kwa ujumla, hatua iliyofikiwa katika sekta ya afya tangu Mapinduzi mwaka 1964 ni makubwa na ya mfano wa kuigwa. Pia kwa mipango iliyopo, ni dhahiri kwamba miaka michache ijayo, kutakuwa na hatua kubwa katika maendeleo ya afya ambayo yatasababisha kuwapo kwa maendeleo kwenye uchumi na kijamii visiwani humo.

AFYA

### MAMBO YA KOREA KUSINI...

# Marufuku kula nyama ya mbwa, yawa ajenda nzito hadi wasomi

**Mwandishi Wetu**

MTU anaweza kujiuliza swali 'mbwa ni mlo sahihi?' Lakini hilo linapoulizwa nchini Korea Kusini linabaki kuwa swali 'butu' kijamii, maana majibu yako wazi.

Ndani ya mazingira ya uenyeji wa nchi hiyo, kuna ufafanuzi unaotolewa kwamba: "Sahani za mbwa huwa ni za wazee wa Korea Kusini, lakini wageni mara nyingi hudhani ni mlo wa kila mtu kwa ujumla."

Park Eun-Kyoung, mtaalamu mshauri anayetumika nchini Ujerumani, anakiri kupata swali hilo kumhoji kuhusu kwao na anafafanua kuna wakati swali hilo humkera.

"Inabeba maana hasi, ikimaanisha kwamba Wakorea wanakula kitu kisichofaa na utamaduni huu ni wa kishenzi," anasema.

Lakini siku za kuuliza maswali kama hayo zinaonekana kuhesabika, kulingana na kile kinachoendelea katika nchi hiyo ya Bara Asia, kikifafanuliwa:

"Mapema wiki hii serikali ya Korea Kusini ilipitisha sheria mpya ya kupiga marufuku ufugaji, uchinjaji, usambazaji na uuzaji wa nyama ya mbwa ifikapo mwaka 2027."

Dai lililopo ni kwamba, itaathiri ustawi katika utamaduni wa karne nyingi zilizopita. Kihistoria, ng'ombe walithaminiwa sana, kama anavyoeleza Dk. Joo Young-ha, Profesa wa Anthropolojia katika chuo ngazi ya cha uzamili katika masomo ya Kikorea.

Hapo ananena pia mbwa walithaminiwa sana na kupata kibali cha serikali, hata wakachinjwa hadi mwishoni mwa karne ya 19.

Inaelezwa kiafya kwamba vyanzo vingine vya protini vilihitajika na kwa wanaoishi pwani Peninsula ya Korea, nyama ya mbwa ilikuwa mojawapo ya chaguo bora zilizofurahiwa na watu katika wigo wa kila tabaka, walikuwapo waliowaepuka.

Kama ilivyo nyama nyinginezo, sahani zinazopendwa kwa kutumia bidhaa ziliibuka, kama vile supu ya nyama ya mbwa inayoitwa "bosintang." Hapo kukawapo vipande vya nyama ya mbwa viliyochemshwa, ukiwa mlo unaosifiwa mtamu na rahisi kula.

Ni tukio lililowashangaza wengi wakati wa michezo ya Olimpiki mjini Seoul mwaka, Korea, Kusini mwaka 1988 wa wakati huo, tukio kubwa la kimataifa ambalo Korea Kusini iliwahi kuandaa na



Nyama ya mbwa inayoandaliwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **Mapema wiki hii serikali ya Korea Kusini ilipitisha sheria mpya ya kupiga marufuku ufugaji, uchinjaji, usambazaji na uuzaji wa nyama ya mbwa ifikapo mwaka 2027.**



ushuhuda wa nyama ya mbwa, ulipoanza kugonga vichwa vya habari duniani.

"Hapo awali watu wengi na hasa wasomi wa kijamii walikasirishwa wakichukua kama kutoheshimu utamaduni mwingine. Hata hivyo, baada ya muda, watu wengi waliona aibu kubaki wakosoaji zaidi," anatamka Dk. Joo.

Kura ya maoni ya mwaka jana, inataja asilimia nane ya wakazi wameshiriki kula nyama ya mbwa (hata walau kwa kuonja), huku miaka minane iliyopita ni asilimia 27 walishiriki.

Takwimu zilizotolewa na Shirika la Korea la Wala Mbwa linaonyesha kupungua kasi ya ulaji nyama ya mbwa, ingawaje bado kuna mashamba takriban 3,000 ya kufuga mbwa nchini Korea Kusini.

Wakati huo huo, inatajwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Masuala ya Vijijini, intamka kwamba umiliki wa wanyama hao umeongezeka na takwimu za uchunguzi za mwaka 2022, ukifafanuliwa uwiano kuna Mkorea mmoja kati ya wanne, walau anakula nyama hiyo.

Mama Yoon Suk Yeol na mumewe Rais Kim Keon Hee, wanatajwa kuwa wapenzi wa wanyama hao wakiwafuga majumbani mwao.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa hadi sasa serikali zote zilizopita nchini Korea Kusini zimeshindwa kutunga sheria kudhibiti mlo huo na kwa serikali ya sasa, pendekezo hilo liko katika wazo kupitiwa upya, kukiendana na ukosoaji kutoka wazo la upande wa pili.

Sheria hadi sasa inamaanisha, baada ya miaka mitatu kupita wanaohusika katika biashara hiyo watakabiliwa na faini au kifungo cha jela ikiwa wataendelea na biashara zao. Hata hivyo, haiharamishi ulaji nyama ya mbwa.

Ni maoni ya kisheria kutoka mzizi wa wanaharakati, akiwamo Jo Hee Kyung, Mkuu wa Chama cha Ustawi wa Wanyama cha Korea (KAWA), amekuwa akifanya kampeni kuhusu suala hilo tangu mwishoni mwa miaka ya 1990.

Marufuku hiyo inatamka chaguo pekee la kukomesha unyanyasaji wa mbwa, huku mwanaharakati huyo akitamka: "Natumai ulimwengu utaacha kuwadhulumu wanyama kwa jina la mila au utamaduni.

"Tunatambua kuwa watu wengi zaidi hawali nyama ya mbwa, ikilinganishwa na wale wanaokula. Tunajua soko linapungua...lakini, bado ni haki yetu kuendesha biashara," anasema Joo Yeong-bong, mfuga mbwa mzoefu na Rais wa Jumuiya ya Kikorea ya Mbwa wa Kula.

Anasema katika kudhibiti bora wa sekta hiyo, hapo awali hapakuwapo chochote na ungeweza kushughulikia masuala mengi ya haki za wanyama.

Kisha, mtaalamu Ahn Yong Geun, Profesa mstaafu wa Uhandisi wa Chakula, katika Chuo Kikuu cha Kitaifa cha Chungnam, maarufu kwa jina 'Daktari wa Nyama ya Mbwa,' naye ana yake,

Akiwa katika watafiti wachache nyama ya mbwa nchini Korea Kusini, alianza kazi hiyo wakati wa Michezo ya Olimpiki ya 1988, nchini humo akiwa anadhaniwa amechanganyikiwa na kile alichohisi ni jibu kwa serikali na wasomi kutoka ukosoaji kigeni.

Kwa sasa, mtaalamu huyo Dk. Ahn, yuko katika ufafanuzi kwamba, faida za kula nyama ya mbwa ina kiwango kidogo cha mafuta na inaweza cha chini cha mafuta na inaweza kutumika kama mbadala wa kiafya kwa nyama kama ya ng'ombe au nguruwe.

Anasisitiza mbwa anaachwa katika historia, hatua anayoihoji inakinzana na uhuru wa kimsingi ulioainishwa katika katiba ya nchi, Korea Kusini, Joo, akisema: "Huwezi kuamuru kile ambacho watu wanaweza kula na wasichopaswa kula."

Maoni hayo yanakinzana na ya Lee Bora, mmiliki wa mbwa kwa miaka sasa, anayepinga kula nyama ya mbwa na anakarinisha sheria mpya kwa mikono miwili ichukue nafasi, akiorodhesha wasiwasi wake kuhusu ulaji wa nyama hiyo.

"Kihisia, natamani watu wasingefuga na kuchinja mbwa kwa ajili ya chakula," anatamka.



## Hospitali ya Dodoma kutumia kondo la uzazi kuzalisha gesi

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma inatarajia kuanza kutumia gesi asilia ambayo itakuwa inazalishwa kitaalamu kwa kutumia masalia ya kondo la uzazi la mama aliyejifungua.

Mwenyekiti wa kitengo cha kusimamia ubora wa huduma za hospitali hiyo, Dk. Edimundi Mgeni, aliyasema hayo wakati akizungumza na Nipashe na kueleza kuwa hatua hiyo itasaidia kupunguza gharama za uendeshaji.

"Hivi sasa kutakuwa hakuna gharama tena ya uchomaji taka za kondo la uzazi badala yake yatahifadhiwa kupitia teknolojia ya kisasa na baada ya kuoza yatatumika kutengeneza gesi asilia ambayo itatumika katika matumizi mbalimbali hospitalini," alisema.

Alisema mfumo huo wa kuhifadhi makondo hayo utaanza kutumika hivi karibuni na itaondoa adha ya kinamama kubeba maji ya moto hospitalini wakati wa kujifungua.

"Tunashukuru serikali kwa kushirikiana nasi kwenye kuhakikisha teknolojia hii inaanza kutumika, ipo tayari itaanza wakati wowote kuanzia sasa, wajawazito hivi sasa hawatakiwi kuja na maji ya moto," alisema.

Naye Ofisa Habari wa hospitali hiyo, Renatha Mzanje, alisema serikali imeendelea kuimarisha huduma za kibingwa katika hospitali hiyo ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

**Alisema mfumo huo wa kuhifadhi makondo hayo utaanza kutumika hivi karibuni na itaondoa adha ya kinamama kubeba maji ya moto hospitalini wakati wa kujifungua.**

# Nishati jadidifu yatajwa kudhibiti athari tabianchi

**Na Mwandishi Wetu**

IMEELEZWA kwamba nishati jadidifu ndiyo suluhisho pekee la kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi pamoja na ukosefu wa ajira kwa vijana.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya CSI Energy Group, Natacha Emilien, aliyasema hayo baada ya kuteuliwa kuongoza kampuni hiyo inayojihusisha na nishati akisema nishati jadidifu inauwezo wa kuzalisha umeme wa uhakika na kutoa ajira.

"Nishati mbadala hunufaisha matabaka yote ya jamii kwa uswa zaidi, hasa wajasiriamali wadogo kutokana na upatikanaji wa nishati kwa bei nafuu, kutoa mafunzo.

"Pia inasaidia katika kushirikiana na wajasiriamali wanawake kama makandarasi wadogo katika mnyororo wa thamani," alisema Natacha.

Akizungumza katika kongamano la mjadala wa kitaifa wa nishati safi ya kupikia uliofanyika Novemba mwaka juzi, Mkurugenzi wa Taasisi ya Climate Action Network Tanzania, Dk. Sixbert Mwanga, alisema utafiti unaonyesha kwamba Tanzania ina kiwango kikubwa cha nishati safi inayotosheleza mahitaji ya wananchi wake.

Alisema nishati jadidifu ni chanzo kingine muhimu kitakachowezesha uzalishaji wa umeme bora kwa bei rahisi na kutosheleza mahitaji ya nchi.

Hivi karibuni Tanzania ilisaini mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu (Irena) ambao utasaidia kupunguza uharibifu wa mazingira unaotokana na uzalishaji wa nishati isiyo rafiki.

Oktoba 31, 2023 Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, alitaja faida za mkataba wa Irene alipokuwa akiwasilisha azimio la mkataba huo bungeni jijini Dodoma.

Dk. Biteko alisema mkataba huo utasaidia kuimarika kwa mchango wa nishati jadidifu katika uzalishaji wa nishati ya umeme na kuliwezesha Taifa kuwa na vyanzo mchanganyiko vya umeme unaoendana na mahitaji ya ukuaji wa kiuchumi na kijamii.

Faida nyingine ni nchi kupata taarifa na takwimu sahihi kuhusu masuala ya nishati jadidifu, fursa za uwekezaji katika nishati hiyo zilizopo, kuimarika kwa utaalamu, teknolojia, utafiti na uelewa kuhusu nishati jadidifu kwa watoa maamuzi na wadau mbalimbali wa nishati.



Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, akiwa amebeba mbuzi beberu aliyezawadiwa na wananchi wa Kijiji cha Lusilile, wilayani Manyoni, mkoani Singida juzi, baada ya kukagua mradi wa maji wa Kintinku-Lusilile ambao utavinufaisha vijiji 13 kikiwamo kijiji hicho. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

## Aweso aagiza kupitiwa upya gharama za kuunganishiwa huduma ya maji

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MANYONI

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amewaagiza wakurugenzi watendaji wa wizara hiyo na bodi za mamlaka za maji kupitia upya gharama za kuunganishiwa huduma ya maji, ili zisiwe kikwazo kwa wananchi.

Alitoa agizo hilo juzi alipokuwa akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Lusilile wilayani Manyoni mkoani Singida baada ya kufanya ukaguzi wa ujenzi wa mradi wa maji wa Kintinku - Lusilile.

Aweso alisema mamlaka hizo kupitia bodi za mamlaka za maji zipitie upya gharama za kuunganishiwa maji kwa kuwa yameanza kujitokeza malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi jambo ambalo serikali isingependa liendelee kujitokeza.

Alisema mamlaka hizo pia zihakikishe suala la ushirikishwaji wa jamii na viongozi katika maeneo ambako miradi inatekelezwa linazingatiwa ili kusiwe na manung'uniko.

Alitumia nafasi hiyo kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha ambazo zimetumika kutekeleza miradi ya maji.

Aidha aliwapongeza watendaji wa sekta ya maji mkoani Singida kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kusimamia miradi ya maji na kuhakikisha huduma ya maji inaimarika.

Mradi wa maji wa Kintinku-Lusilile utakapokamilika utahudumia wananchi zaidi ya 55,000 kutoka vijiji 11 wilayani Manyoni mkoani Singida, utagharimu Sh.bilioni 13.

# DUWASA kuchimba visima 16 kwa bil.1.19/-

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

KATIKA kukabiliana na upungufu wa maji katika Jiji la Dodoma, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) inachimba visima 16 katika maeneo ya Nzuguni na pembezoni mwa Jiji hilo, gharama ikiwa ni Sh.bilioni 1.19.

Meneja Miradi kutoka DUWASA, Mhandisi Norbert Mwombeki, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa juu ya mkakati wa kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji.

Alisema visima hivyo vitaongeza kiwango cha uzalishaji wa maji na kuboresha hali ya upatikanaji wa maji kwa Jiji la Dodoma kutokana na kukua kwa kasi.

"Jiji la Dodoma ni miongoni mwa majiji yanayokua kwa kasi hivyo kufanya mahitaji ya maji kuwa makubwa kwa sasa mahitaji halisi yanakadiriwa kuwa zaidi ya lita milioni 133 na uzalishaji kwa sasa ni lita milioni 79.6," alisema.

Aidha, alifafanua kuwa DUWASA imekamilisha uchimbaji wa visima viwili na kati ya vitano katika eneo la Nzuguni vilivyogharimu Sh. milioni 260.

"DUWASA inaendelea na uchimbaji wa kisima kikubwa na kirefu cha maji cha mfano katika eneo la Nzuguni, ambapo uchimbaji wake umefikia mita 253 kati ya mita 300 zitakazochimbwa na utagharimu Sh. milioni 570 mpaka kukamilika kwake," alisema.

Alisema uchimbaji wa kisima hicho cha mfano una lengo la kufikia tabaka la maji katika kina kirefu zaidi kuwahi kufikiwa kwa Jiji hilo.



# RC atoa siku 21 wanafunzi waliofaulu kuripoti shuleni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ametoa wiki tatu kwa viongozi wa Wilaya ya Chunya kuhakikisha wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu wanaripoti shuleni.

Homera alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na wanahabari kuhusu hali ya usajili wa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari mkoani hapa.

Alisema ikiwa sasa ni wiki ya pili tangu shule zifunguliwe bado hali ya wanafunzi wa kidato cha kwanza kuripoti shuleni ndani ya mkoa huo siyo ya kuridhisha kwa maelezo kuwa idadi kubwa ya wanafunzi bado hawajaripoti.

Alisema mpaka sasa ni asilimia 38 pekee ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari ndiyo walioripoti shuleni, huku zaidi ya asilimia 62 wakiwa bado mitaani.

Homera alisema Halmashauri ya Jiji la Mbeya ndiyo ambayo inaongoza mkoani Mbeya kwa wanafunzi kuripoti shuleni kwa zaidi ya asilimia 81 ikifuatiwa na Wilaya ya Kyela yenye asilimia 62 ya wanafunzi walioripoti. Homera alisema kuwa Wilaya ya Chunya inaburuza mkia kwa kuwa na asilimia 18 pekee ya wanafunzi wake waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza ambao wamesharipoti.

"Nitumie fursa hii kutoa wiki tatu kwa Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mkurugenzi na Ofisa Elimu wa Halmashauri hiyo kushughulikia suala hilo na kuhakikisha wanafunzi wote wanaripoti shuleni vinginevyo itanibidi niwachukulie hatua," alisema Homera.

Alisema hakuna sababu ya wanafunzi kutoripoti shuleni kwa wakati kwa kuwa wanaruhusiwa kuanza masomo hata kama hawajakamilisha mahitaji ya shule kama vile nguo za shule, madaftari na vitu vingine ambavyo wanapaswa kuwa navyo.

Hata hivyo Homera alisema kuwa mbali na kufuatilia wanafunzi hao na kuwataka waripoti shuleni haraka, mkoa pia unaandaa ripoti nyingine ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule za serikali, lakini wazazi wao wakawaondoa na kuwapeleka kwenye shule za watu binafsi.

"Tunatambua kuwa miongoni mwa wale wanafunzi tuliowachagua kwenye shule zetu za serikali wapo ambao wazazi wao wameshawapeleka katika shule za watu binafsi na hivyo kuonekana kwenye takwimu zetu kuwa hawajaripoti shuleni, hawa nao tunawafanyia kazi ili tujue idadi yao na kuwatolea taarifa," alisema Homera.

Hivi karibuni Kamati ya Bunge ya Serikali za Mitaa ilipofanya ziara yake mkoani Mbeya ilionyesha kukerwa na hali ya wanafunzi kutoripoti shuleni na kutoa maelekezo kwa Mkuu wa Mkoa kuhakikisha wanafunzi hao wanakwenda shuleni.

Katika maelekezo yake, kamati hiyo ilimtaka Mkuu wa Mkoa kupitia upya orodha ya mahitaji ya wanafunzi wakiamini kuwa huenda ndiyo yakawa kikwazo kwa wazazi kuwapeleka watoto shuleni.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Denis Londo alisema yapo maelekezo ya jumla ya vitu ambavyo wanafunzi wanatakiwa kuwa navyo wanaporipoti shuleni na kwamba kuna uwezekano baadhi ya shule zikawa na maelekezo ya ziada.



Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mbeya, Mwalimu Juma Mageni, akizungumza na wanafunzi wa kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Iziwa, jijini Mbeya alipokuwa kwenye ziara ya kufuatilia mahudhurio ya wanafunzi kwenye shule mbalimbali jijini humo, hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## DC awaomba viongozi wa dini kuhamasisha usafi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIONGOZI wa dini mkoani Mbeya wametakiwa kutoa elimu ya usafi wa mazingira kwa wananchi ili kuepuka magonjwa ya mlipuko kikiwamo kipindupindu ambacho kimesharipotiwa kwenye baadhi ya mikoa.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa alitoa ushauri huo juzi alipozungumza na waumini wa Kanisa la Efatha wakati wa ibaada maalumu ya kuliombea taifa iliyofanyika katika Kanisa Kuu lililopo Forest Mpya jijini Mbeya.

Alisema wananchi wanatakiwa kufundishwa kunawa mikono mara kwa mara kwa kutumia majisafi na sabuni na kuhakikisha wanaosha matunda kabla ya kula.

"Tumekisikia kipindupindu huko Mwanza, Shinyanga na kule Kagera, huku kwetu hatuna kisa chochote lakini ni lazima tuanze kujihami maana ugonjwa huu huwa unasambaa kwa kasi kubwa sana," alisema Malisa.

Alisema kipindi hiki cha mvua ugonjwa huo huwa unasambaa kwa kasi zaidi na hivyo akawataka wananchi kuhakikisha wanachemsha maji ya kunywa na kutumia dawa.

Malisa alisema viongozi wa dini wanaaminika na waumini wao kiasi kwamba wakiwahamasisha ni rahisi kuelewa na kutekeleza kuliko mtu mwingine akiwaeleza.

**Alisema wananchi wanatakiwa kufundishwa kunawa mikono mara kwa mara kwa kutumia majisafi na sabuni na kuhakikisha wanaosha matunda kabla ya kula.**

## Wanafunzi 9,356 kati ya 21,356 Njombe waripoti shuleni

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANAFUNZI 9,356 kati ya 21,356 waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka huu mkoani Njombe sawa na asilimia 43.9 wameripoti shule za sekondari walizopangiwa.

Hayo yalielezwa na Ofisa Elimu Mkoa wa Njombe, Nelasi Mulungu, wakati wa ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka ya kutembelea shule za sekondari Lunyanywi na Mpechi.

Mulungu alisema hadi kufikia Januari 15 wanafunzi 9,356 pekee ndiyo walioripoti shuleni, huku 12, 000 wakiwa bado hawajaripoti, ambapo hatua mbalimbali zimeanza kuchukuliwa.

"Tumejaribu kuongea na viongozi wote, wakuu wa wilaya wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa kuwashirikisha viongozi wa kata, watendaji wa kata, wenyeviti wa vijiji mpaka vitongoji kuhakikisha kwamba watoto wote ambao wamefaulu mtihani wanaingia kidato cha kwanza," alisema Mulungu.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Mpechi, Brown Kiswaga, alisema shule hiyo kwa sasa haina changamoto yoyote, hivyo aliwaomba wazazi kuwapeleka shule watoto waliopangiwa hapo.

"Wazazi waleteni watoto wenu waliopangiwa hapa kwa sababu hakuna changamoto Rais (Samia Suluhu Hassan) ameboresha miundombinu ya kusomea, waacheni watoto waje shule," alisema Kiswaga.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Kuruthum Sadick, alisema hakuna mtoto atakaye achwa nyumbani ilihali amefaulu hivyo hatua kali zitachukuliwa kwa wazazi watakaokaidi kuwapeleka watoto shule.

"Miundombinu imeboreshwa, serikali imeleta fedha nyinyi niwaombe wazazi mlete watoto shule msikae nao majumbani kwa sababu elimu ndiyo mkombozi pekee kwa mtoto kuweza kufikia ndoto zake," alisema Sadick.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, alisema hakuna sababu ya mzazi kutompeleka shule mtoto ilhali ameondoa vikwazo vingi.

"Wazazi wote wenye watoto wanafunzi niwaombe wawatoe watoto majumbani ili watoto wote waje mashuleni lakini jambo lingine niwaombe sana wazazi kama una mtoto ni mwanafunzi na wakati huu ni wakati wa kuwa darasani tusaidiane kwenye malezi kuhakikisha kwamba watoto hawatoroki," alisema Mtaka.

Baadhi ya wanafunzi akiwamo, Warid Danda alitoa wito kwa wanafunzi wenzake kuzingatia masomo ili kufaulu vizuri kwa sababu serikali imeboresha miundombinu.





## Ethiopia, Tanzania zakubaliana kuimarisha uchumi, diplomasia

**Na Elizabeth Zaya**

ETHIOPIA na Tanzania zimekubaliana kushirikiana katika kuimarisha uchumi na diplomasia.

Makubaliano hayo yametokana na mazungumzo yaliyofanywa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Mambo ya Nje wa Ethiopia, Demeke Hassen.

Viongozi hao walifanya mazungumzo hayo juzi walipokutana kwenye mkutano wa Jukwaa la Uchumi Duniani (WEF), unaofanyika Davos, Uswisi.

Pia Dk. Mpango alifanya mazungumzo na Mkurugenzi wa Taasisi ya Global Plastic Action Partnership, Clemence Schidm na kuikaribisha taasisi hiyo kushirikiana na Tanzania katika kukabiliana na taka za plastiki.

Kadhalika walikubaliana kufanya utafiti utakaowezesha kutambua aina ya taka zinazopatikana kando ya bahari na maeneo ya nchi kavu ili kusaidia kuandaa mkakati wa kukabiliana na changamoto hizo.

Dk. Mpango aliikaribisha taasisi hiyo kushirikiana na Tanzania katika kudhibiti taka za plastiki hususani mkoani Dodoma kwa kuanzisha miradi itakayowezesha uchakataji wa taka na utenganishaji wa taka za plastiki.

Dk. Mpango alisema ni vema kuandaa jukwaa la kimataifa kuhusu uchakataji wa taka za plastiki litakalowakutanisha wakusanya taka wa ndani ya nchi na kampuni za kimataifa zinazojihusisha na shughuli hizo ili kujadili na kupata uzoefu kutoka katika kampuni hizo.

Makamu wa Rais anamwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan, katika mkutano huo uliolenga kujadili masuala mbalimbali, ikiwamo uchumi na uwekezaji, utawala bora, usalama wa chakula, mabadiliko ya tabia ya nchi pamoja na kilimo.

Mkutano huo ulifunguliwa juzi na Rais na mwanzilishi wa jukwaa hilo, Prof. Klaus Schwab, ukifuatiwa na hotuba kutoka kwa Rais wa Uswisi, Viola Amherd.

WEF umehudhuriwa na wakuu wa nchi na serikali kutoka mataifa mbalimbali, watendaji wakuu wa mashirika ya kimataifa, wakuu wa taasisi na kampuni mbalimbali pamoja na wafanyabiashara.

# Wasiojulikana wang'oa vibao vya mitaa, namba za nyumba

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Kamati Kuu ya Kitaifa ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwanza 2022, Kassim Majaliwa amesema baadhi ya wananchi wameanza kung'oa vibao vya utambulisho wa majina ya mitaa na namba za nyumba nchini na kurudisha nyuma maendeleo ya nchi.

Majaliwa aliyasema hayo jana katika kikao cha 10 cha kamati hiyo kilichofanyika visiwani hapa.

Alisema taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Tanzania Bara na Visiwani zinatakiwa kufuatilia na kuhakikisha vibao vya anuani za majina ya mitaa nchini havihujumiwi na kubakia katika uhalisia wake ili kumrahisishia mwananchi kufika sehemu husika bila usumbufu.

Alizitaka serikali za mitaa kuweka sheria ambazo zitatoa adhabu kwa mtu atakayebainika kuharibu miundombinu hiyo iliyowekwa na serikali kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi hasa kuhusu sensa ya watu na makazi.

Alizitaka Serikali za Mitaa kuhakikisha wanapotoa vibali vya ujenzi kwa wananchi kugawa na namba za nyumba ili kurahisisha upatikanaji wa maendeleo na serikali kufikia malengo yake ya kuwapatia huduma muhimu kupitia takwimu za sensa ya watu na makazi.

Majaliwa ambaye ni Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alisema taarifa za sensa ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa ambazo hutumika katika kutambua matukio yanayotokea katika jamii.

Alitolea mfano namna taarifa za sensa zilivyosaidia kutambua idadi ya watu walioathirika katika maporomoko ya udongo yaliyotokea katika Kijiji cha Katesh Wilaya ya Hanang' mkoani Manyara na kusababisha watu kadhaa kufa, kujeruhiwa na nyumba kufukiwa na udongo.

Mwenyekiti Mwenza wa Kamati hiyo ambaye ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla alisema serikali imeridhika na namna viongozi wa serikali walivyotoa ushirikiano kufanikisha Sherehe za Miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka huu zilizofanyika wiki iliyopita visiwani hapa.

Alisema jambo hilo linadhihirisha uimara wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambao umedumu kwa miaka mingi.

Kwa upande mwingine, alipongeza kamati hiyo kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya ambayo inaonyesha ni jinsi gani viongozi wamekuwa wazalendo wa nchi yao kuwarahisishia wananchi kupata mahitaji na huduma stahiki kwa urahisi zaidi.

Hemedi aliwataka viongozi kuwa mstari wa mbele kuzisaidia serikali zote mbili katika kuleta maendeleo kwa wananchi kupitia takwimu za sensa hiyo mijini na vijijini.

Wajumbe wa kamati hiyo wamezitaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Tume ya Taifa ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) kuhakikisha zinatumia matokeo ya sensa hiyo hasa ya umri na jinsia kwa ajili ya kuhuisha kwenye daftari la wapigakura ili watu wote wenye sifa za kupiga kura waandikishwe na kupata haki yao ya msingi ya kuchagua na kuchaguliwa katika chaguzi zijazo.




Sehemu ya wananchi na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wakifuatilia hotuba ya Mwenyekiti wa Taifa wa Chama hicho, Rais Samia Suluhu Hassan, alipohutubia, baada ya kuweka jiwe la ufunguzi wa Tawi la CCM Chaani Masingini, Mkoa wa Kaskazini Unguja jana, akiwa katika ziara ya kukagua miradi mbalimbali ya chama. **PICHA: IKULU**

# Bidhaa feki zapungua Zenji, Bara

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limesema ushirikiano baina yake na Shirika la Viwango Zanzibar (ZBS) umesaidia kupunguza kuwapo kwa bidhaa zisizokuwa na viwango kutoka Zanzibar kwenda Bara.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Athuman Ngenya kwenye maonyesho ya biashara yanayofanyika Nyamanzi nje ya mji wa Zanzibar.

Dk. Ng'enya alisema shirika hilo limeshiriki maonyesho hayo kwa ajili ya kuelimisha na kueleza umma mafanikio ambayo TBS limepata miaka 60 iliyopita.

Alisema moja ya mafanikio makubwa ni ushirikiano baina yake na ZBS. "Ilikuwa ni muhimu kuwa na ushirikiano huu kwa sababu biashara kati ya visiwani (Zanzibar) na bara ni kubwa sana na zinahusiana na bidhaa mbalimbali ambazo zinadhibitiwa viwango na TBS na ZBS, kwa hiyo mnaweza kuona umuhimu wa kuwa na ushirikiano huo," alisema Ngenya.

Alisema ushirikiano huo umewezesha kupunguza bidhaa ambazo hazina ubora baina ya pande hizo mbili za Muungano na kuongezeka ubora.

Mtaalamu wa Lishe na Kiongozi wa Jumuiya ya Wenye Viwanda Vidogo Tanzania (WAJATA), Issa Njoka alipongeza TBS kwa kuhudumia Watanzania na kuimarisha viwanda kwa kuhakikisha vinazalisha bidhaa bora ambazo zinalinda afya za watumiaji.

Njoka ambaye alitembelea banda la TBS kwenye maonyesho hayo, alisema kama mzalishaji wa bidhaa zinazotokana na kilimo amepata huduma na maelekezo ya kina kutoka kwa maofisa wa shirika hilo waliokuwa wanatoa elimu kwa wananchi.

"Lakini nimeweza kuelewa kuwa kila Mtazania na wazalishaji kwa ujumla wanatakiwa wafike TBS ili waelimishwe ni namna gani wanaweza kupata bidhaa bora ili pale unapokuwa unakula kitu lazima kiwe kimethibitishwa na TBS," alisema Njoka na kuongeza;

"Ni lazima Watanzania tuwe wazalendo tunapotaka kununua bidhaa ni lazima kuangalia kama ina alama ya ubora ya TBS ili kuepuka kula bidhaa zenye madhara kiafya ambazo zinaweza kusababisha ukapoteza maisha."

Alisema kwenye vyakula zinapatikana sumukuvu na nyingine, hivyo kila Mtanzania ajione ni sehemu ya TBS. "Natoa wito kwa kila Mtanzania kuitumia TBS ili kuweza kuboresha bidhaa zetu kupitia shirika hili," alisema Njoka.

Aliwataka wazalishaji kuhakikisha wanatengeneza bidhaa zenye ubora ili waheshimike kwani wakiitumia TBS wanalijengea sifa taifa kuwa lina viwanda na bidhaa bora.

# Mtambo kutengeneza noti bandia wakamatwa Goba

**Na Julieth Mkireri**

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani limekamata mtambo wa kutengenezea fedha bandia Goba, jijini Dar es Salaam.

Kukamatwa kwa mtambo huo kumetokana na mahojiano kati ya watuhumiwa waliokamatwa na fedha bandia huko Msata wilaya ya kipolisi Chalinze na washirika wengine waliobainika baadaye mmoja wao akiwa mkazi wa Goba.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo, alisema mtambo huo ulikamatwa katika makazi ya mmoja wa watuhumiwa baada ya upekuzi uliofanywa na jeshi hilo.

Pia zilikamatwa kompyuta, gundi, jiki, tina, rangi, visu na bunda la karatasi zikiwa katika hatua ya kutengeneza fedha hizo bandia.

Kabla ya kukamatwa mtambo huo Januari 10, katika Kijiji cha Msata, watuhumiwa walikamatwa na fedha bandia za kitanzania noti 155 za Sh. 10,000.

Kamanda Lutomo alisema fedha hizo zenye thamani ya Sh. 1,550,000 zilikamatwa na watuhumiwa Mbaraka Miraji (54) na Zena Issa (42), wakazi wa Buza, jijini Dar es Salaam.

Alisema kukamatwa kwa watuhumiwa hao kumefanikishwa na mmoja wa raia wema baada ya kutilia shaka noti ya Sh. 10,000 aliyoipokea kwa malipo ya huduma katika nyumba ya kulala wageni huko Msata.

Baada ya mahojiano polisi ilibaini washirika wao Masumbuko Paul (54), mkazi wa Goba na Elias Wandiba (50), mkazi wa Kimara Suka, jijini Dar es Salaam wakiwa na fedha nyingine zenye thamani ya Sh. 12,000,000 za noti za Sh. 10,000, 5,000 na 2,000.

Polisi imetahadharisha wananchi kuwa makini na fedha wanazopokea kutoka kwa watu.



Mkuu wa Wilaya ya Tanga, James Kaji ambaye ni Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Muheza, akizungumza na askari polisi kata, baada ya kumalizika kwa kikao kazi mjini Muheza juzi. Kulia kwake ni Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai wa wilaya hiyo, Charles Ntenga. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Anayetuhumiwa kumuua mkewe anaswa Mtera

**Na Ibrahim Yassin,** KYELA

MWIMBAJI maarufu wa kwaya kwenye kanisa moja la kiroho kijiji cha Ikulu, Kata ya Ipinda wilayani Kyela mkoani Mbeya, Aliko Mwakalibule (38), anayetuhumiwa kumuua mkewe Metrida Kyoma (22) kwa kumkata na panga amenaswa akiwa bwawa la Mtera, mkoani Iringa.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Ikulu, Brasto Mwandunga, alisema mtuhumiwa alitenda kosa hilo Januari mosi, mwaka jana baada ya kutoka naye kwenda kunywa pombe kijiji jirani cha Kafundo wakiwa na mtoto wa miaka minne.

Alisema usiku saa nne wakati wakirejea nyumbani, walipita njia ya mkato kwenye vichaka akiwa na kusudio la kutenda kosa hilo baada ya kuficha panga kichakani walikokuwa wanapita na kumkata sehemu mbalimbali mkewe na kusababisha kifo chake.

"Kijana huyo ni mtanashati muumini wa kanisa la kiroho na muimba kwaya maarufu ameshangaza watu juu ya mauaji hayo, kabla ya kutekeleza mauaji aliuza uwanja akanunua panga akalificha kichakani, fedha zingine alizitenga kwa ajili ya safari ya kutoroka," alisema Mwandunga.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Ikulu, Jackson Mwang'onda, alisema baada ya kupigiwa simu na Mwenyekiti alifika eneo hilo na kupiga simu polisi na kumchukua mwanamke huyu akiwa hajiwezi ambaye alifariki wakiwa njiani kuelekea hospitali.

Alisema mtuhumiwa alikuwa na wivu wa kupindukia kwa kuwa alikuwa na ugomvi na mkewe kila akimwona anasalimiana na mwanamume ilikuwa ni shida na huyo alikuwa mwanamke wa tano kuishi naye baada ya wanne kuachana nae kwa nyakati tofauti kutokana na vitendo vyake.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Ipinda, Ally Joel alisema baada ya tukio walianzisha msako kwa kuweka mitego sehemu mbalimbali hadi ilipofika jana walipopatiwa taarifa kuwa yupo Migoli kwenye Bwawa la Mtera linalotumika kwa uvuvi wa samaki.

Alisema baada ya kupata taarifa hizo kwa kushirikiana na uongozi wa Migoli na Jeshi la Polisi walimnasa na kumweka rumande na taratibu za kumsafirisha kwenda Kyela zinaendelea.

Alisema katika kijiji cha Ikulu hilo ni tukio la pili mfululizo, kwa siku za hivi karibuni Erasto Kikali (43), alikamatwa na polisi kwa tuhuma za kumuua mkewe kwa kipigo kwa kumpaka sumu ya kuulia magugu mdomoni huku chupa hiyo akiiweka pembezoni mwa mwili ili ijulikane alijiua.

Alisema uchunguzi wa madaktari ulibaini marehemu hakunywa sumu bali aliuawa kwa kipigo baada ya kuona alama za uvimbe mgongoni.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Josphine Manase, alisema wamekuwa wakitoa elimu mara kwa mara ili kumaliza vitendo hivyo na kwamba wanaume wengi wamekuwa wakiwajeruhi wake zao kwa wivu wa mapenzi na kukimbilia nchini Malawi.

Alisema kutokana na matukio hayo, wataendelea kutoa elimu zaidi kuanzia ngazi za vitongoji, vijiji, kata na tarafa kupinga vitendo hivyo.

Kamanda wa Polisi mkoani Iringa, Alan Bukumbi, akizungumza kwa njia ya simu alisema bado hajapewa taarifa na Mkuu wa Polisi wilaya na kwamba atalizungumzia kwa kina sakata hili atakapopewa taarifa ili taratibu za kumsafirisha mtuhumiwa kwenda Kyela zifanyike.


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AMRANY HAMIDU MLAWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 378 AEK – TOYOTA LJ95R GKMNS** yenye Chassis namba **LJ950006982.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **SOG/RB/14/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ANGELINE EMMANUEL MUNISI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 110 CPE – TOYOTA LITEACE NOAH** yenye Chassis namba **SR 400146698,** Engine namba **355087520.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/PWA/BAG/3919/2023.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**ESTER EDSON MWAKAGALI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0203/0028** kilichotolewa na IRINGA GIRL'S SECONDARY mwaka 2017. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0214/0540** kilichotolewa na MSALATO SECONDARY mwaka 2020. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/MBE/CHU/8649/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**GS GROUP** inatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 720 CUH** aina ya **HAOJUE HJ125-8EX.** Chassis namba **LC6PCJK24M0022286.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **SOG/RB/74/2024.**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Bukoba,**

**Kituo cha Bukoba Mjini Mkoa wa Kagera**

**Shauri la Madai Na. 182/2023**

**Jina la Mdai ......................KIKUNDI CHA UJIMA – BUNUKANGOMA**

**Jina la Mdaiwa ....................REMIGIUS LAURIAN**

**KUITWA SHAURINI KWA MDENI MHUKUMIWA KWA REMIGIUS LAURIAN**

Kwamba mdai ameleta maombi mbele ya Mahakama hii kwa ajili ya utekelezaji wa hukumu ya shauri tajwa hapo juu. Unatakiwa kufika mbele ya Mahakama hii tarehe 24 Mwezi 01 Mwaka 2024 kueleza kwa nini hukumu isitekelezwe dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama leo tarehe 10 Mwezi 01 Mwaka 2024.

MAHAKAMA YA MWANZO WILAYA YA BUKOBA BUKOBA MJINI

RESIDENT MAGISTRATE BUKOBA URBAN PRIMARY COURT

**HAKIMU**

# Mchungaji Paul Mackenzie akabiliwa na mashtaka 10

**NAIROBI,** Kenya

MKURUGENZI wa mashtaka nchini Kenya Renson Ingonga ameidhinisha mashtaka 10 dhidi ya mchungaji mwenye utata Paul Mackenzie wa Kanisa la Good News International, anayetuhumiwa kusababisha vifo vya watu zaidi ya 430 eneo la Shakahola pwani ya nchi hiyo.

Mchungaji Mackenzie hivi karibuni alituhumiwa na kashfa ya kuwalazimisha waumini wa kanisa lake kufunga hadi kufa ili waende kukutana na Mungu.

Pia Mahakama Kuu mjini Malindi iliupa upande wa mashtaka siku 14 kufanya tathmini ya afya ya akili kwa Paul Mackenzie na washtakiwa wengine 30 kabla ya kusomewa mashtaka kwa madai ya mauaji ya watu wengi huko Kilifi.

Kiongozi huyo wa mashtaka alieleza jana kuwa baada ya kutathmini faili la uchunguzi kutoka idara ya upelelezi alibaini kwamba kuna ushahidi wa kutosha wa kumshtaki mchungaji Mackenzie na washirika wake 95 wanaohusishwa na vifo vya washirika wa kanisa hilo la kufunga hadi kufa.

Ilielezwa kuwa baadhi ya mashtaka dhidi ya Mackenzie ni mauaji, ugaidi pamoja na kuua bila kukusudia na kusababisha majeraha ya mwili.

Kwa mujibu wa sheria ya Kenya ya kuzuia ugaidi na uhalifu wa kupangwa, watuhumiwa hao watashtakiwa kwa kuhusika kwenye uhalifu wa kupangwa na mafunzo yenye itikadi kali.

Aidha, chini ya sheria ya kuwalinda watoto Mackenzie na washirika wake watakabiliwa na kosa la ukatili dhidi ya watoto na ukiukaji wa haki ya kupata elimu.

Hata hivyo Mackenzie na watuhumiwa wenzake wamekuwa mahabusu kwa zaidi ya miezi saba tangu mwezi Mei 2023 hadi sasa. **RFI**

# Mlipuko waathiri vitongoji Nigeria

**ABUJA,** Nigeria

MLIPUKO mkubwa umetokea katika mji wa Ibadan nchini Nigeria na kuua watu wawili na kujeruhi 77 usiku wa kuamkia jana. Na kwamba jitihada za uokoaji zinaendelea katika vitongoji saba vya jiji hilo lenye idadi kubwa ya watu.

Inaelezwa kuwa chanzo cha mlipuko huo bado hakijafahamika, lakini mamlaka inashuku kuwa huenda ulichochewa na vilipuzi vya uchimbaji madini vilivyohifadhiwa ndani ya nyumba. Huku picha zikionyesha majengo yaliyogeuzwa vifusi na magari yaliyoharibiwa na mlipuko.

Pia ilielezwa kuwa polisi waliahidi kufanyika uchunguzi wa haraka kuhusu mlipuko huo, huku shahidi mmoja akielezea duka moja kuharibiwa katika Wilaya ya Bodija.

"Tunasikia kishindo kikubwa saa 7:30 usiku na maduka ya Dominoes Pizza na Ace Mall huko Bodija ziliharibiwa," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa huo, Seyi Makinde, alisema "Uchunguzi wa awali wa vyombo vya usalama umebaini kuwa wachimbaji haramu waliokuwa wakimiliki moja ya nyumba huko Bodija walikuwa wamehifadhi vilipuzi vilivyosababisha mlipuko huo".**BBC**



Maofisa wa uokoaji wakiwa katika eneo lililokumbwa na mlipuko jana Nigeria. **PICHA: MTANDAO**

# Trump anapoendeleza jitihada kugombea urais

**WASHINGTON,** Marekani

BAADA ya Rais wa zamani wa Marekani, Donald Trump, kuibuka mshindi kwenye uchaguzi wa mapema wa kuidhinisha mgombea urais wa Republican, kwa kujipata asilimia 51 ya kura zilizopigwa, macho yote sasa yanaelekezwa kwenye jimbo la New Hampshire ambako uchaguzi utafanyika.

Inaelezwa kuwa jimbo la New Hampshire litafanya uchaguzi wa awali wa kumwidhinisha mgombea wa urais wa Chama cha Republican, Jumanne ya wiki ijayo.

Aidha, katika uchaguzi uliopita uliofanyika katika Jimbo la Iowa wapinzani wa Trump walishindwa kwa asilimia kubwa akiwamo Gavana wa Florida Ron DeSantis akiwa na asilimia 21.2 ya kura zilizopigwa, akifuatiwa na Gavana wa South Carolina Nikki Haley, ambaye alipata asilimia 19.1, na mfanyabiashara Vivek Ramaswamy akiwa na asilimia 7.7.

Wawaniaji watatu wa chama hicho, Trump, Desantis na Nikki Haley, ndio watakaoshindana wiki ijayo, baaada ya muwaniaji wa nne, Vivek Ramaswamy kujiondoa kutokana na uchaguzi wa Jumatatu. Huku wengine wote wakitajwa kupata chini ya asilimia moja ya jumla ya kura zilizopigwa.

Hata hivyo inaelezwa kuwa ushindi huo unampa motisha Trump kwenye uchaguzi sawa na huo utakaofanyika New Hampshire, ambako Haley amekuwa akipata umaarufu mkubwa, kwa matumaini kwamba ataweza kushinda na kuleta mwamko mpya kwenye kampeni za Republican.

Vile vile ilielezwa kuwa mara ya mwisho kwa Trump kushiriki kwenye uchaguzi wa Iowa ilikuwa 2016 alipokuwa akitafuta uteuzi wa rais, ambapo alishindwa na Seneta wa Texas Ted Cruz, wakati huo akijipatia asilimia 24.3 ya jumla ya kura zilizopigwa.

### MASHTAKA YAMZONGA

Ilibainisha kuwa licha ya ushindi alioupata Trump, pia anatarajiwa leo kuwasili New York baada ya kushtakiwa na Jean Carroll kwa mara ya pili katika mahakama ya kiraia kwa kumkashifu, na kwamba mwaka 2023 alimshtaki kwa mara ya kwanza kwa tuhuma za unyanyasaji wa kijinsia.

Inaelezwa kuwa Trump alitangaza nia yake ya kwenda kujitetea ana kwa ana katika chumba cha mahakama dhidi ya Jean kutokana na mashtaka hayo.

Trump alisema hajawahi kumuona mwanamke huyo maishani mwake (...) na hajui yeye ni nani, akisisitiza mwanamke huyo ni muongo, licha ya kuelezwa kuwa mwezi Mei ilitolewa hukumu ya kumlipa Jean dola milioni tano kwa unyanyasaji wa kijinsia unaodaiwa kufanyika mwaka 1996, huku kashfa hiyo ikiibuliwa 2022.

Wakili wa mlalamikaji, Roberta Kaplan, alimwandikia hakimu akieleza wasiwasi wake kwamba upande wa Chama cha Republican ungegeuza kesi hiyo kuwa sarakasi na kutaka kuzua fujo.

Ilielezwa kuwa kesi hiyo itakayosikilizwa leo kwa uteuzi wa majaji, inatarajiwa kudumu kwa siku kadhaa, na kwamba ni kitendo cha pili cha aina yake.

Mei 9, 2023, majaji 12 wa mahakama ya kiraia ya Manhattan kwa kauli moja waliamua kwamba Trump alihusika na shambulio la kijinsia kwa Jean, mnamo 1996, katika chumba cha duka kuu la New York, na kwamba pia alimkashifu Oktoba 2022.

Majaji walimhukumu Donald Trump, ambaye alikata rufani na hakuwahi kufunguliwa mashtaka ya jinai katika kesi hiyo, kwa fidia ya dola milioni tano, zaidi ya Sh.bilioni 12.5.

Ilielezwa kuwa Jean pia aliwasilisha malalamiko ya kukashifiwa kwa taarifa za awali za Trump, mwezi Juni 2019, kufuatia tuhuma zake za kwanza za ubakaji zilizomo kwenye kitabu.

Inabainishwa kuwa mwanamke huyo anatafuta angalau fidia ya dola milioni 10, sawa na Sh. bilioni 25 kwa madhara yake ya kimaadili na kitaaluma. **VOA, RFI**

# MNUNKA HATARI AKIIBEBA SIMBA QUEENS LIGI KUU

**Na Oliver Albert**

AISHA Mnunka, mshambuliaji wa Simba Queens ana balaa, ndivyo unavyoweza kusema kwa jinsi anavyozidi kuonyesha kiwango bora katika Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake Tanzania, inayoendelea.

Mshambuliaji huyo ambaye alisajiliwa na Simba Queens Juni mwaka, 2021 akitokea Alliance Girls ya Mwanza, hivi sasa ndiye kinara wa mabao katika ligi akiwa amepachika wavuni magoli nane huku pia akiongoza kwa kufunga hat-trick, nyota huyo tayari ana hat-trick mbili.

Mchezaji huyo alifunga hat-trick yake ya pili juzi na kuiongoza timu yake kutoka nyuma na kupata ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Amani Queens.

**Mabao hayo yamemfanya Aisha kuwa kinara wa ufungaji akifuatiwa na Winfrida Gerald na Stumai Abdallah wote kutoka JKT Queens ya Dar es Salaam, kila mmoja akiwa amefunga mabao sita.**

Msimu huu umeonekana kuanza vizuri kwa Aisha ambaye amekuwa akianza katika kikosi cha kwanza mara kwa mara tofauti na msimu uliopita ambapo alikaa benchi mara nyingi, hivyo kumaliza msimu akiwa na bao moja tu.

Kocha Msaidizi wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', amefurahishwa na kiwango cha nyota huyo huku akimtaka kuendelea kupambana kwa ajili ya timu na yeye binafsi.

"Amekuwa na kiwango bora tangu kuanza kwa msimu, ndio maana tumeendelea kumpa nafasi ya kucheza na amethibitisha kwa kufanya ambacho benchi la ufundi linataka.

"Muhimu asibweteke, aendelee kupambana kwa ajili ya timu kwa sababu msimu huu tunataka kurudisha heshima ya Simba kwa kutwaa ubingwa, " alisema Mgosi.

Akizungumzia mchezo wao dhidi ya Amani ambao ilibidi watoke nyuma kwa mambo 2-1 na kupata ushindi wa mabao 3-2, Mgosi alisema ulikuwa mchezo mgumu.

"Mchezo ulikuwa mgumu sana kwa sababu Amani Queens wana wachezaji wazuri kwa sasa na hiyo imetuonyesha hatutakiwi kubweteka lazima tujiandae sana kwa michezo mingine ijayo ili kutimiza malengo yetu, " alisema Mgosi.

Michezo mingine iliyochezwa juzi, Yanga Princess ililala kwa bao 1-0 dhidi ya Ceasiaa Queens, JKT Queens iliichapa Alliance Girls mabao 5-0, Baobab Queens ilitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Fountain Gate Princess wakati Bunda Queens iliinyuka Geita Gold Queens mabao 2-0.



Mshambuliaji wa Simba Queens, Aisha Mnunka (kulia), akipokea mpira kutoka kwa mwamuzi, Amina Kyando, baada ya kufunga hat-trick katika mechi ya Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake Tanzania dhidi ya Amani Queens iliyochezwa kwenye Uwanja wa Ilulu, Lindi. Simba Queens ilishinda mabao 3-2. **PICHA: SIMBA SC**

# Umakini tatizo kubwa Yanga Princess

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga Princess, Charles Haalubono, ameilalamikia safu ya ulinzi na ushambuliaji kukosa umakini uliosababisha kupoteza alama tatu dhidi ya Ceasiaa Queens katika mechi ya Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi.

Bao pekee katika mechi hiyo lilifungwa na Janeth Matulanga dakika ya 60.

Akizungumza na gazeti hili, Haalubono, alisema kipindi cha kwanza walifanikiwa kutengeneza nafasi lakini wachezaji wake walishindwa kuzitumia vyema na kusababisha kukosa mabao.

Kocha huyo alisema hata baada ya kurejea dakika 45 za mwisho safu yake ya ulinzi ilifanya makosa ambayo wapinzani wao waliyatumia kuwaadhibu na kuondoka na alama tatu katika mchezo huo.

"Tumepoteza mechi kwa kukosa umakini, mchezo ulikuwa wa ushindani mkubwa tumepata nafasi tumeshindwa kuzitumia na wachezaji wangu na tumeona mapungufu tunarudi uwanja wa mazoezi kufanyia kazi na kujiandaa na mchezo ujao," alisema kocha huyo.

Aliongeza anahitaji wachezaji wake kuongeza umakini katika michezo iliyopo mbele yao huku akisikitika kupoteza mechi mbili mfululizo.

Yanga Princess yenye pointi tisa ilipoteza mchezo dhidi ya watani zao, Simba Queens.

## Ukata sababu nyota kukimbia Singida FG

**Na Saada Akida**

RAIS wa Singida Fountain Gate FC, Japhet Makau, amesema changamoto ya kukosa fedha ndio imesababisha wachezaji wake tegemezi kuondoka lakini pia wanahitaji kumalizana na nyota wengine ambao wanaidai timu hiyo, imeelezwa.

Makau aliliambia Nipashe amelazimika kuuza baadhi ya wachezaji ndani na nje ya nchi ili kupata fedha zitakazowasaidia kukamilisha mchakato wa kuwalipa wachezaji waliovunja mikataba yao na kusababisha kufungiwa kusajili na Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA).

Rais huyo alisema katika siku za hivi karibuni kumetokea sintofahamu na mambo mengi kuhusu timu yao lakini ameweka wazi wanapambana kuhakikisha wanaondoka na changamoto zinazowakabili.

"Tutajipanga kuhakikisha mambo yanarudi katika utaratibu mzuri, ni kweli baada ya kufanya biashara ya kuwauza baadhi ya nyota wetu, fedha zinazopatikana zitakwenda moja kwa moja kutatua changamoto tulizonano, tunaahidi kurejesha timu yenye ushindani," Makau alisema.

Aliongeza wameshaanza kufanya mazungumzo na nyota wengine ambao kwa ajili ya kuziba nafasi zilizoachwa na nyota walioondoka na kukiongezea kikosi nguvu.

"Singida Fountain Gate FC kazi yetu ni soka na hatuna sehemu ya kuingizia fedha zaidi ya mpira wa miguu kwa kuuza baadhi ya wachezaji na kuongezea tulizopata katika vyanzo vingine ili kutatua changamoto tulizokuwa nazo.

Uamuzi wa kuuza baadhi ya wachezaji ambao wako katika kiwango bora ulitokana na kuhitaji fedha, lakini kuuza nyota wetu hao hatuwezi kuathiri timu yetu katika mipango yetu ya kufanya vizuri katika Ligi Kuu na mashindano mengine yaliyopo mbele yetu," alisema Makau.

Aliongeza uamuzi wa mchezaji yupi aondoke ulifanywa kwa kulishirikisha benchi la ufundi linaloongozwa na Kaimu Kocha Mkuu, Thabo Senong, ambaye alitoa baraka katika kukamilisha mchakato huo.

"Kocha Thabo alishirikishwa na kuridhia kuondoka kwa baadhi ya wachezaji wetu ili kupata fedha na tujipange na usajili wa dirisha kubwa la usajili. Tunatarajia hadi kufikia Aprili, mwaka huu tutakuwa tumemalizana na wachezaji wote wanaotudai, sasa tayari tumeshamalizana na nyota wawili ingawa hatuwezi kuweka wazi majina yao kwa sasa," aliongeza rais huyo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### AIT-NOURI ANUKIA EPL

ARSENAL na Liverpool zimeonyesha nia ya kumsajili beki wa kushoto wa Wolves na Timu ya Taifa ya Algeria, Rayan Ait-Nouri, 22. ***(Football Transfers)***

### ALCANTARA NJIA MOJA

LIVERPOOL wanataka kusalia na kiungo wa kati wa Hispania, Thiago Alcantara, 32, lakini mchezaji huyo amezivutia Flamengo ya Brazil na Al-Ettifaq ya Saudi Pro League. ***(Teamtalk)***

### NEWCASTLE KUJIPANGA UPYA

KLABU ya Newcastle wanaenda kukagua mipango yao ya uhamisho wa Januari katika mkutano maalum wiki hii kufuatia jeraha la kiungo wa kati wa Brazil, Joelinton, 27. ***(Guardian)***

### YAMKATAA GYOKERES

CHELSEA haina nia ya kumnunua mshambuliaji wa Sporting CP na Sweden, Viktor Gyokeres, 25, licha ya ripoti za ofa ya pauni milioni 73 kuwekwa kwa mchezaji huyo. ***(Football London)***

### REGULION KUTUA SPURS

BRENTFORD imefanya makubaliano ya mdomo na Tottenham Hotspur kwa ajili ya kumnunua kwa mkopo beki wa kushoto wa Hispania, Sergio Reguilon, 27, ingawa hakuna kipengele cha chaguo la kununua kwa mkataba wa kudumu. ***(Fabrizio Romano kupitia X)***

### MBAPPE MKATABA MNONO

KLABU ya Paris St-Germain imeripotiwa kumpa mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe, 25, mkataba mpya wenye thamani ya euro milioni 100 kwa msimu ili kujaribu kumbakiza. ***(AS kupitia Mirror)***

### ZIRKZEE ATAJWA UNITED

KLABU ya Manchester United inamlenga mshambuliaji wa Bologna, Joshua Zirkzee, 22, msimu wa joto. ***(Florian Plettenberg)***

### WOLVES YAMFUATA BROJA

KLABU ya Wolves inafikiria kumnunua Armando Broja, 22, ambaye mustakabali wake unategemea iwapo Chelsea itasajili mwezi huu. ***(Guardian)***

### MOURINHO KUREJEA PORTO

JOSE Mourinho, anaweza kurejea katika usimamizi na klabu yake ya zamani ya FC Porto baada ya kutimuliwa na AS Roma Jumanne. ***(Express)***

### SOARES KUTUA ARSENAL

ARSENAL ipo katika mazungumzo na Besiktas kuhusu dili la kumnunua mlinzi wa Timu ya Taifa ya Ureno, Cedric Soares, 32. ***(Mail)***

### TRAORE, CHAMBERS KUONDOKA

MSHAMBULIAJI wa Burkina Faso, Bertrand Traore na mlinzi wa England, Calum Chambers, wanazivutia klabu za Ulaya baada ya kuambiwa wanaweza kuondoka Aston Villa katika dirisha la Januari hii. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




## NYOTA BARCELONA WAMVURUGA XAVI

### Ni kutokana na viwango wanavyoonyesha katika mbio...

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernández, anapambana kuwaweka wachezaji upande wake huku sehemu ya kikosi cha kwanza ikipoteza imani naye, kwa mujibu wa ESPN.

**Barca ilichapwa mabao 4-1 na Real Madrid katika fainali ya Supercopa ya Hispania iliyochezwa Jumapili iliyopita, lakini vyanzo vinasema kukatishwa tamaa kulitangulia kushindwa kwa Clásico huko Saudi Arabia.**

Wachezaji kadhaa wamekuwa wakihoji mbinu za timu kwa muda, pia wamekerwa Xavi alisema hawajaweza kuzoea mtindo wa uchezaji wa Barca. Chanzo kimoja cha habari kilisema sio wachezaji wote wana maoni sawa, lakini wengine wanahisi amekuwa hana ukali kwa baadhi ya nyota wa kikosi hicho.

Chanzo kilicho karibu na Xavi kinasisitiza hisia za kocha huyo ni wachezaji bado wako naye, huku kikikiri kuna uwezekano wachezaji wengi kutokuwa na furaha.

Wanatambua matokeo hayajatarajiwa hadi sasa msimu huu, lakini wanasema Xavi amefurahishwa na tabia iliyoonyeshwa na timu nzima.

Ushindi wa 3-2 dhidi ya Almeria kabla ya Krismasi ulitajwa na chanzo kimoja kama "badiliko" katika uhusiano kati ya wachezaji na kocha.

Xavi alisema baada ya mchezo huo alitoa mazungumzo magumu zaidi ya timu yake wakati wa mapumziko huku Barca wakijitahidi kupata ushindi kwa bao la ushindi dakika ya 83 kutoka kwa Sergi Roberto dhidi ya klabu ya mwisho ya LaLiga, ambayo haijashinda msimu huu.

Hata hivyo, ingawa wakati huo umetajwa, mashaka yamezuka hapo awali Barca ilipopata kichapo kwenye LaLiga dhidi ya Madrid na Girona na kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Shakhtar Donetsk na Royal Antwerp.

Xavi amesema katika mikutano kadhaa ya wanahabari anaamini uhusiano na wachezaji wake bado ni mzuri. Akizungumza baada ya kushindwa na Madrid, alisema bado anawaamini na anaamini wanaweza kubadilisha msimu.

Wakati huo huo, Mkurugenzi wa Michezo, Deco, alisema "haina maana" kuhoji hatima ya Xavi, akiongeza kocha huyo, ambaye hivi majuzi alisaini mkataba mpya hadi 2025, aliendelea kuungwa mkono na klabu hiyo.

Lakini vyanzo vya ESPN havijasema wazi, vikikubali kwamba kuna mashaka juu ya mustakabali wa Xavi zaidi ya msimu huu, licha ya kuongezewa mkataba huo.

Hilo linaonyesha imani inapungua, lakini hali ya usawa ya kifedha ya Barca inafanya ngumu kumfukuza Xavi na kuteua mbadala wake.

Vyanzo viliongeza iwapo Xavi ataondoka kabla ya msimu kuisha mchezaji wa zamani wa kimataifa wa Mexico, Rafa Marquez, ndiye chaguo linalopendekezwa na Rais, Joan Laporta, kuchukua nafasi yake kwa muda.

Kipigo cha Jumapili kutoka kwa Madrid kilikuza uchezaji mbaya wa hivi majuzi wa Barca, ambao haujawahi kuadhibiwa kulingana na matokeo lakini umekosolewa na vyombo vya habari vya ndani.

Wameporomoka kwa pointi nane nyuma ya vinara wa LaLiga, Girona, ambao wamecheza mechi moja zaidi, na wapo pointi saba nyuma ya Madrid, wanaoshika nafasi ya pili.

## HABARI MICHEZO



# BENZEMA AMSHTAKI WAZIRI UFARANSA

**PARIS,** Ufaransa

NYOTA wa Ufaransa, Karim Benzema, amewasilisha kesi mahakamani ya kuharibiwa jina dhidi ya Waziri wa Mambo ya Ndani wa Ufaransa kwa kumtuhumu ana uhusiano na Kundi la Muslim Brotherhood, vyombo vya habari vya nchini humo vimeripoti.

Waziri, Gérald Darmanin, alisema mnamo Oktoba, mwaka jana Benzema “ana uhusiano mbaya” na Kundi la Kiislamu la Sunni.

Maoni hayo “yanadhoofisha” heshima na sifa yake, wakili wa Benzema alisema.

Kundi la Muslim Brotherhood limepigwa marufuku katika nchi kadhaa zikiwamo Misri, Urusi na Saudi Arabia.

Maoni ya Darmanin ya Oktoba yalikuja baada ya mchezaji huyo kuandika kwenye ukurasa wake wa Twitter anaunga mkono watu wa Gaza kama “waathiriwa tena wa mashambulizi ya kidhalimu ya mabomu ambayo hayawaachi wanawake wala watoto”.

Alisema Benzema alishindwa kuonyesha huruma kama hiyo kwa waathirika 1,300 wa Israel waliouawa na Hamas Oktoba 7, mwaka jana. Darmanin alisema mshambuliaji huyo wa zamani wa Ufaransa “anajulikana sana kwa uhusiano wake na Muslim Brotherhood”.

“Tunapambana na zimwi ambalo ni Muslim Brotherhood, kwa sababu inajenga mazingira ya jihadi,” mwanasiasa huyo alikiambia kituo cha televisheni cha kihafidhina cha CNews.

Benzema mwenye umri wa miaka 36, ambaye anacheza Saudi Arabia na alikanusha haraka madai hayo na kutishia kuchukua hatua za kisheria dhidi ya waziri huyo kwa kashfa.

## Aziz Ki, Diarra watakata AFCON

**ABIDJAN,** Ivory Coast

NYOTA wawili wa Yanga, Stephane Aziz Ki na Djigui Diarra wameonja ladha ya michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), vyema baada ya kuanza vizuri kwenye kikosi cha kwanza katika timu zao taifa.

Aziz Ki alianza kwenye kikosi cha Burkina Faso kilichokuwa kinacheza na Mauritania na alikuwa mmoja wa wachezaji walioonyesha kiwango cha kuvutia kwa kutupia mashuti kadhaa.

Katika mchezo huo uliochezwa mapema, Burkina Faso waliibuka na ushindi wa bao 1-0 lililofungwa kwa penalti dakika za majeruhi na Bertrand Traore.

Aziz Ki alionekana kuwa nguzo muhimu kwa kikosi cha Burkina Faso katika safu ya kiungo na ushambuliaji.

Kwa upande wa mchezo wa usiku uliozikutanisha Afrika Kusini na Mali, golikipa namba moja wa Yanga, Diarra naye alikuwa kwenye kikosi cha kwanza.

Katika mchezo huo, ambao Afrika Kusini ilianza kwa kupata penalti dakika za mwanzo, lakini mshambuliaji wake, Percy Tau aliipaisha.

Na hivyo ikawafanya Afrika Kusini waadhibiwe kwa kufungwa mabao 2-0 yakifungwa na Hamari Traore and Lassine Sinayoko, huku Diarra akiokoa hatari nyingi zaidi langoni mwake.

Mashuti manne ambayo yalionekana kama yangekuwa bao, yote yaliokolewa kwa ustadi mkubwa na Diarra na alionekana kutulia zaidi langoni mwake.

Hata hivyo, bila uwezo binafsi wa Diarra pengine Afrika Kusini wangeweza nao kupata angalau bao katika mchezo huo.

Katika mchezo mwingine, Tunisia ilifungwa na Namibia bao 1-0 likifungwa na Deon Hotto kwa kichwa dakika ya 88.




## Osimhen: Nitacheza EPL siku za baadaye

**ABIDJAN,** Ivory Coast

MSHAMBULIAJI wa Napoli, Victor Osimhen, amethibitisha nia yake ya kutaka kucheza katika Ligi Kuu England (EPL), kwa siku zijazo, lakini amesisitiza kujitolea kwake kwa timu yake ya sasa.

Osimhen analengwa kwa muda mrefu na Chelsea, ambayo inatafuta suluhisho ya matatizo yao ya ufungaji kwa mwaka huu, huku Arsenal pia inajulikana inamtaka mchezaji huyo wa kimataifa wa Nigeria, ambaye hivi karibuni alisaini mkataba mpya na Napoli ambao unajumuisha kipengele cha kutolewa chenye thamani ya zaidi ya pauni milioni 100.

Kuongezewa kwa mkataba wake kulionekana kutokuwa na uhakika mwanzoni mwa msimu huu wakati Osimhen alipotumiwa ujumbe wa matusi katika mtandao wa kijamii kutoka akaunti ya Napoli, lakini mvutano ulipunguzwa na Osimhen akasaini mkataba mpya.

“Nina furaha na Rais wa Napoli,” alisema Osimhen akiiambia Sky Sport.

“Nina uhusiano mzuri naye, siwezi kusema uongo, amekuwa nami tangu niliposaini katika klabu hii mwaka, 2020. Nina uhusiano mzuri na familia yake pia. Siku zote ni muhimu kwangu kuhakikisha hakuna kitu kibaya, bila kujali kilichotokea na uhusiano na yeye na familia yake.

“Amekuwa akiniunga mkono nje ya uwanja na bila shaka najitolea kwa bidii kushinda Scudetto nikiwa nao.”

Alipoulizwa kuhusu uwezekano wa kuhamia England, Osimhen alikiri: “Ni kweli siku moja, bila shaka, lakini kwa sasa nina mipango mingine katika kazi yangu. Wakati utakapofika, kila mtu atajua.”

Osimhen hapo awali alikiri alikuwa na jezi za Chelsea na Manchester United alipokuwa mtoto, ingawa alikataa nafasi ya kusajiliwa na Mashetani Wekundu mwaka 2020.

Sasa akiwa mmoja wa washambuliaji bora duniani, Osimhen anawaniwa na klabu nyingi, lakini bei yake bila shaka itapunguza timu ambazo zinaweza kufanya makubaliano ya kumsajili.

Chelsea wanatarajiwa kuendelea na harakati zao za kumnasa Osimhen baada ya dirisha dogo la usajili la Januari, huku Arsenal pia wakitafuta chaguo lao la mshambuliaji.

HABARI MICHEZO

# TECNO kuwapatia viatu wenye vipaji

Na Mwandishi Wetu

KAMPUNI ya uzalishaji wa simu aina ya TECNO imezindua kampeni ya 'Busti Kipaji' yenye lengo la kutoa viatu kwa watoto wenye uhitaji ambao wana vipaji vya kucheza mpira wa miguu, imeelezwa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mkufunzi wa Kampuni ya TECNO, Shakila Mkima, alisema mdau anayetaka kuchangia katika kampeni hiyo atachangia kwa kununua simu aina ya TECNO Spack 20 na kwa kufanya hivyo, utakuwa umemsaidia mtoto mmoja.

Mkima alisema uzinduzi wa kampeni hiyo ni mwendelezo wa dhamira ya kampuni yao kuleta athari chanya kwa jamii ya Watanzania.

"Wadau na mashirika mbalimbali wanatakiwa kuunga mkono kwa dhati juhudi hii, akisema pamoja tunaweza kuleta tofauti kubwa katika maisha ya watoto wenye vipaji nchini," alisema Mkima."

Aliweka wazi kampuni yao inawaalika watu wote kujiunga na kampeni hiyo kwa kununua simu ambapo kila ununuzi, TECNO itatoa viatu vya michezo kwa mtoto mwenye uhitaji.

"Juhudi hii ya ushirikiano unalenga kuwawezesha kizazi cha vijana kukuza ndoto na matarajio yao kupitia furaha ya michezo. Kwa kutambua hamasa kubwa iliyopo kwenye michezo kwa sasa, TECNO leo (jana), tunawatambulisha rasmi Ofisa Habari wa Simba, Ahmed Ally na Msemaji wa Yanga, Ali Kamwe, kuendesha kampeni hii ya Busti Kipaji kusaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu," aliongeza.

Kwa upande wake, Ahmed, alisema watoto wengi wanashindwa kutimiza ndoto zao kutokana na kukosa viatu na vifaa vya kuchezea na hata wakipata wanashindwa kutumia kutokana na kuzoea kucheza bila viatu.

"Tunaomba wadau na mashirika mbalimbali kuunga mkono kwa dhati juhudi hii, kwa pamoja, tunaweza kuleta tofauti kubwa katika maisha ya watoto wenye vipaji nchini," Ahmed aliongeza.

Naye Kamwe alisema ni vizuri kusaidia watoto ili watimize ndoto zao kupitia vipaji kwa sababu mpira wa miguu ni mchezo namba moja duniani unaoweza kubadilisha maisha ya mtu.

# GAMONDI AONGEZA DOZI YA MAZOEZI YANGA SC

Na Saada Akida

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi amesema amelazimika kuongeza dozi ya mazoezi kwenye kikosi chake ili kuendana na wachezaji waliopo kwenye fainali za AFCON pindi watakaporejea kikosini hapo.

**Gamondi, amesema ameangalia mechi za AFCON na kugundua wachezaji wanajituma na kupambana sana kwa ajili ya timu zao hivyo wakirejea kutoka huko watakuwa kwenye viwango vikubwa.**

Kocha huyo amesema hiyo ndio sababu ya kuongeza dozi kwa wachezaji alionao kikosini kwa kuwafanyisha mazoezi mara mbili kwa siku ili wawe fiti zaidi.

"Kwa jinsi nilivyoona michuano ya AFCON, wachezaji wote wa timu yangu ambao wapo huko na vikosi vyao vya taifa wanaongeza vitu vingi ikiwamo ufundi, pumzi na fiziki, hivyo nataka na waliobaki nao wasikae bure au kufanya mazoezi mepesi kwani hawatokuja kuwa sawa, hii ndio sababu ya kuongeza muda wa mazoezi," alisema Gamondi.

Akizungumza na Nipashe, Gamondi alisema licha ya Ligi Kuu Tanzania Bara kusimama kupisha Fainali za AFCON timu yake haitakuwa na muda wa kupumzika kwa sababu wanatambua wanakibarua kigumu mbele yao kwa michezo ya Ligi na mashindano ya Kimataifa.

Alisema baada ya mapumziko mafupi walipotoka katika michuano ya Mapinduzi sasa wamerejea kutengeneza timu ili kuweka muunganiko na wachezaji wapya ambao wamesajiliwa kipindi cha dirisha dogo la usajili.

"Tunaendelea na mipango yetu kwa sababu bado kazi kubwa ipo mbele yetu, ukiangalia wachezaji baadhi walikuwa kwenye mapumziko mafupi hawakuwapo katika Kombe la Mapinduzi, tumerejea mapema kuweza kujipanga kwa muda huu wachezaji wapya wameingia wanahitaji kuzoea timu ili tufikie malengo," alisema Gamondi.

Aliongeza kuwa anahitaji wachezaji wake wote kuwa vizuri kwa sababu wanamichezo migumu mbele yao ikiwamo ya ligi ambapo baada ya ligi kurejea wataanza kwa kucheza na JKT Tanzania kabla kukutana na CR Belouizdad ya Algeria kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika.

Alisema wamefanya usajili kulingana na mahitaji yake kwa kufanyia kazi mapungufu aliyoyaona kwenye kikosi chake na sasa kikosi kimekamilika.

Kikosi cha Yanga kwa sasa kinafanya mazoezi mara mbili asubuhi jioni kwenye uwanja wa Avic Town, Kigamboni.




Msemaji wa Yanga, Ali Kamwe (kushoto) na Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, wakionyesha viatu ambavyo watapewa wachezaji vijana wenye vipaji ambao ni wahitaji maalumu kupitia Kampeni ya Busti Kipaji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## *Simba SC mpya baada...*

INATOKA UK. 24

mabeki wenye nguvu, Baleke mwanzoni alikuwa hivyo lakini inaonekana sasa amekuwa mwepesi sana, sijui amemkubwa na nini, halafu anakosa sana mabao, hilo lilikuwa halimfurahishi sana kocha," alisema mtoa habari huyo ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini kutoka ndani ya uongozi wa timu hiyo.

Chanzo hicho kilisema, Banchikha tangu amefika hakuridhishwa na viwango vya Baleke na Phiri na kupelekea kuagiza uongozi kufanya mchakato wa kupata washambuliaji wengine.

"Watu wanalalamika tu, lakini namba haziongopi kwa siku za karibuni tumekuwa tukikosa mabao mengi au hatufungi kabisa, Simba siyo timu ya kucheza dakika 90 na Mlandege bila kupata bao, kocha alikasirika sana na akachukua maamuzi hayo magumu, alisema kama na Mlandege tu inakuwa hivyo, je na timu kubwa za Afrika kwenye Ligi ya Mabingwa itakuwaje?" Kiongozi huyo alibainisha.

Alisema kocha huyo atapitisha tena panga lake mwishoni mwa msimu na uwenda wachezaji wengine wenye majina makubwa wakaachwa msimu ujao.

Mbali na Phiri na Baleke, wengine waliopigwa panga na Kocha Benchikha ni Jimmson Mwanuke, Nassor Kapama, Mohamed Mussa na Shaaban Chilunda.

## Moloko aondoka

INATOKA UK. 24

kubwa namna mashabiki wanavyopenda vilabu na wachezaji wao, hili ni jambo la kujivunia sana Watanzania," alisema Moloko.

Aliongeza anarudi nchini kwao kuanza maisha mapya ya soka na kila kitu kitajulikana baada ya kufika huko kwa sababu bado ana uwezo wa kucheza soka kwa kiwango cha juu.

„Nitaendelea na maisha ya soka, kwa sasa narudi Congo (DRC), kujipanga, na najua nitapata timu muda ukifika, bado nitaendelea kucheza soka," Moloko aliongeza.

Winga huyo pia ameushukuru uongozi wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na wachezaji wenzake kwa ushirikiano waliompatia katika muda wote akiwa ndani ya timu hiyo.

Michezo
Alhamisi Januari 18, 2024
Nipashe



Nyota Barca wamvuruga Xavi

UKURASA 21



Golikipa wa Timu ya Taifa ya Mali na Yanga, Djigui Diara, akishangilia baada ya timu yake kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Afrika Kusini kwenye mchezo wa kwanza wa kundi E katika Fainali za AFCON zinazoendelea nchini Ivory Coast. Aliisaidia timu yake kuibuka na ushindi huo baada ya kudaka mkwaju wa penalti uliopigwa na Percy Tau anayeichezea klabu ya Al Ahly ya Misri. **PICHA: MTANDAO**

# Simba mpya baada ya kuwatema sita

**Adam Fungamwango na Faustine Feliciane**

## ●●● Benchikha ahusika kwenye usajili dirisha dogo, aandaa mauaji, Julio...

USAJILI uliofanywa na Simba kwenye dirisha dogo la usajili inaelezwa kwa asilimia 90 umefanywa na kocha wa timu hiyo Abdelhak Benchikha ikiwa ni sehemu ya kukiunda upya kikosi cha timu hiyo.

**Uamuzi wa kuwaondoa kikosini nyota sita na kusajili wengine watano kumeleta sintofahamu kwa baadhi ya mashabiki lakini hayo ni maamuzi ya kocha huyo ambaye anataka kuiunda Simba ya 'mauaji'.**

Maamuzi hayo ya Kocha Banchikha yameungwa mkono na kocha wa zamani wa timu hiyo, Jamhuri Kiwhelu 'Julio' ambaye ametaka kocha huyo aachwe afanye kazi yake na baadaye aje kuhukumiwa kwa matokeo atakayoyapata.

Julio alisema soka la sasa makocha ndio wanaofanya usajili au kupendekeza wachezaji wa kusajiliwa kutokana na matakwa ya mbinu na mfumo wake anaotaka kuutumia.

"Nadhani wamuache kocha afanye kazi yake, yeye ndio anajua ni mchezaji gani anamtaka ambaye anaweza akampa matokeo kutokana na mbinu zake, lakini pia ndio anaamua mchezaji gani haachwe kutokana na kutokwenda na kasi yake yake," alisema Julio.

Habari kutoka ndani ya Simba zinasema kuwa pamoja na kwamba inaonekana wanachama na mashabiki wengi hawajafurahishwa kuondoka kwa baadhi ya nyota hao, lakini inaelezwa kuwa Benchikha ndiye mwenye sauti ya mwisho kwenye benchi la ufundi na ameamua hivyo bila kuingiliwa na mtu au kiongozi yeyote.

Mtoa taarifa alisema kama ingekuwa ni amri ya viongozi ingekuwa ngumu kuwatoa washambuliaji wawili (Baleke na Phiri) kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili na angalau wangesubiri hadi mwishoni mwa msimu, lakini tangu wakati anapewa timu, alikabidhiwa mamlaka ya kufanya chochote anachokiona kinafaa kwenye benchi la ufundi kwa manufaa ya timu.

"Mmemsikia wenyewe baada ya Kombe la Mapinduzi amesema haridhishwi na washambuliaji waliopo kikosini, akasema kama kweli Simba inataka kwenda mbele na angalau kufanya vyema kwenye mechi za Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa ni lazima viongozi wamtafutie mshambuliaji mwenye sifa za kuwa mkatili langoni, mwenye nguvu za kuweza kukabiliana na

INAENDELEA UK. 23

# Moloko aondoka na faili la Ligi Kuu Bara moyoni

**Na Faustine Feliciane**

ALIYEKUWA winga wa Yanga, Jesus Moloko, amesema anaondoka Tanzania huku akiwa na kumbukumbu nzuri ya ushindani uliopo katika Ligi Kuu Bara.

Rasmi Yanga juzi ilitangaza kuachana na winga huyo kwa makubaliano ya pande zote baada ya kudumu katika kikosi chao kwa muda wa miaka mitatu.

Akizungumza na Nipashe jana, Moloko, alisema hataisahau Ligi Kuu Tanzania Bara kutokana na ushindani wake lakini pia mapenzi ya mashabiki kwa klabu zao na wachezaji.

„Nimeishi vizuri sana hapa Tanzania, sitaisahau ligi ya hapa, imekuwa na ushindani, na ki-

INAENDELEA UK. 23



Moloko

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002